# Nipashe

Jumamosi Machi 11, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581246

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT

TZS. 1,087,305,640

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#





**ACT:** Serikali ichukue hatua, kukabili baa la njaa nchini

UKURASA 3




UKURASA 11

## KESI YA KINA MDEE

# Maswali 30 yalivyoibua siri kortini



Dk. Azaveri Lwaitama

**• Mbowe** alimwita Mdee Nairobi, alilia... *Endelea Ukurasa 2*



Waombolezaji, waandishi wa habari, ndugu, jamaa na marafiki wakilishusha kaburini jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Mwandishi na Mwakilishi wa gazeti la Nipashe Kanda ya Ziwa, Richard Makore, wakati wa maziko yake kijijini kwao Remng'orori wilayani Serengeti mkoani Mara jana. Makore alifariki dunia Machi 7 mwaka huu kwa ajali ya basi la Sheraton mkoani Geita akiwa katika safari ya kikazi. **PICHA: VITUS AUDAX**

## Chongolo: Mabosi wazembe watawekwa pembeni

UKURASA 18

## Mhasibu benki atekwa, achomwa moto porini

UK.18


**SPECIAL SUPPLEMENT ON COMPLETION OF TWO YEARS UNDER THE ABLE LEADERSHIP OF**



**HER EXCELLENCY DR. SAMIA SULUHU HASSAN**

The Guardian Limited will publish a special supplement with **"The Guardian"** and **"Nipashe"** Newspapers, with a special report focusing on the achievements of the Government under the leadership of President **Dr. Samia Suluhu Hassan**

**20th March 2023**

We wish to invite you to be a part of this special supplement by publishing your **Special features, Congratulatory messages, Advertorials** and **Advertisements.**

The Guardian Nipashe

**TO BOOK YOUR SPACE PLEASE CALL US TODAY ON +255 677 020 701**

Email: advertise@guardian.co.tz or Visit us at The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Opposite ITV / Radio One, Dar es Salaam Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com

617309101



**MICHEZO** SIMBA KUNGURUMA MANUNGU UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Maswali 30 yalivyoibua siri

**Na Grace Gurisha**

MCHUANO wa maswali yenye majibu zaidi ya 30 kwenye Mahakama Kuu Masjala Kuu Dar es Salaam katika kesi inayowahusu wabunge 19 wanaopingwa na chama chao cha CHADEMA uliibua ulingo wa umahiri, mambo ya siri na kipekee kizimbani jana.

Wakati maswali ya waleta maombi, Ipilinga Panya, yakipata majibu ya papo kwa hapo na ufafanuzi wa umahiri, simulizi za siri zikianikwa kizimbani, hata wakili anakumbushwa na Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini ya CHADEMA, Dk. Azaveri Lwaitama, kurejea yale aliyomfunza akiwa mwanafunzi wake.

Ni aina ya mjadala kisheria ambao kuna wakati Jaji Cyprian Mkeha, alihisi hoja zao zinavuka mipaka, hata akaingilia kati huku akiwaonya.

Ni kesi ambayo Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee na wenzake 18 walifungua shauri Julai 22 mwaka jana wakiiomba mahakama ipitie mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama na kisha itoe amri ya kuwahalalisha.

Dk. Lwaitama ambaye kwa sasa ni mhadhiri mwandamizi katika chuo kikuu, alidai mahakamani atakuwa mtu wa kwanza kuwatetea kurudishwa kwenye chama endapo watatoka bungeni na kufuata utaratibu.

Mjumbe huyo alikuwa anajibu maswali ya dodoso toka kwa Wakili Panya baada ya kuchezwa kwa video inayomwonesha Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe anazungumza.

Dk. Lwaitama alidai Mbowe alikuwa anazungumza kwamba alimwita Mdee jijini Nairobi, Kenya ili kuzungumza naye kwa kile ambacho walichokifanya kwa kuwa yeye (Mdee) ndiye kiongozi wa wenzake kutokana na ushawishi mkubwa aliokuwa nao.

Alidai kuwa Mbowe baada ya kuzungumza na Mdee, mbunge huyo alilia, hivyo kama watatoka leo bungeni, yeye atakuwa mtu wa kwanza kuwatetea kurudishwa kwenye chama kwa kuwa shida sio ubunge wao, bali utaratibu haukufuatwa.

"Utaratibu waliotumia ni batili na wa kihuni, kwa sababu haiwezekani mtu atoke gerezani usiku, aghushi barua halafu aende akaapishwe, hiyo sio sahihi kabisa," alidai Dk. Lwaitama

**Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano hayo kortini jana:**

**Panya:** Ikitokea katiba ya vikundi imekwenda kinyume na Katiba ya nchi, wewe utaifuata ipi?



Dk. Azaveri Lwaitama

**Lwaitama:** Nitaifuata Katiba ya nchi kwa sababu ninaiheshimu na ndio maana ninachukia watu wanaoweka watu bungeni ambao sio wanachama.

**Panya:** Wewe unapinga hawa waleta maombi kuwa sio wabunge au unapinga kuwa hawakuteuliwa na chama chako?

Lwaitama: Sasa hilo swali gani? Hawa sio wabunge kwa mujibu wa Katiba.

**Panya:** Hawa waleta maombi 19 wamekoma kuwa wanachama wa CHADEMA lini?

**Lwaitama:** Pale chama kilipopeleka barua kwa Spika wa Bunge kuwa wamekoma kuwa wanachama.

**Panya:** Mahakama na sisi tunataka kujua ni lini hiyo barua imepokewa?

**Lwaitama:** Taarifa zilizopo kwenye kiapo changu zinajitosheleza.

**Panya:** (Alimpatia kiapo chake kinzani ili akisome kwa ajili ya kujua tarehe barua ilipofika kwa Spika). Tarehe hiyo hauijui?

**Lwaitama:** Hilo hitimisho umelipata wapi? Sijaelewa huyu mwanafunzi wangu, mimi nilikufundisha kutembea na taarifa kichwani? Nenda katafute hizo taarifa, mimi sio Mtendaji Mkuu wa chama, hata kuwa ninahifadhi kila kitu.

**Panya:** Hiyo barua iliyokwenda kwa Spika kutoka kwa chama kwa uelewa wako ilikwenda kwa spika kabla hawa hawajawa wabunge au baada ya wao kuwa wabunge?

**Lwaitama:** Ilikuwa baada ya wao kutenda kitendo hicho cha kuapa, acha kutafuta ujanja kuwatetea watu.

**Panya:** Kwa kipindi hicho kabla ya barua walikuwa wabunge?

**Lwaitama:** Ndiyo na ndiyo maana kuna watu wanasema ni wabunge wa mchongo.

**Panya:** Ule mchakato wa ndani wa kuwapata watu wanaokwenda kuwa wabunge, ulifuatwa au haukufuatwa?

**Lwaitama:** Kuteua na kukokotoa na baadaye kuwaeleza kuwa ninyi ni wabunge na hii inakuja baada ya uchaguzi, wananchi wanapigia wagombea kura na tume inachakata kura na kuleta orodha.

**Panya:** Swali langu, ule mchakato wa ndani ya chama ulifuatwa au haukufuatwa?

**Lwaitama:** Ndiyo ulifuatwa.

**Panya:** Kuna dhana ambayo waleta maombi 19 wanasema kwenye maombi yao kuwa wanashangaa na kugeukwa kuwa wao wanasema walifuata utaratibu na kuna shahidi anaitwa Hanje aliwahi kusema hilo.

**Wakili Jeremiah Mtobesya:** Jaji; hilo swali lina matatizo. Linamtaka shahidi atoe maoni kwenye ushahidi wa shahidi mwingine.

**Jaji:** Hebu rudia swali.

**Panya:** (Anarudia swali)

**Lwaitama:** Utaratibu wanaosema ulifanyika ni ule wa mchakato wa kupata majina ya viti maalum wa chama ngazi zote na utaratibu walikiuka kupeleka hayo majina kwa tume kinyume cha utaratibu wa chama.

**Panya:** Wewe ulipata wapi hayo kuwa hao walipeleka majina bila baraka za Kamati Kuu?

**Lwaitama:** Niliyajua kwenye kikao cha Baraza Kuu lilikosikiliza rufani zao, na hayo yapo pia kwenye huo muktasari wa kikao cha Kamati Kuu.

**Panya:** Wewe ulikuwa mjumbe wa Kamati Kuu?

**Lwaitama:** Kwani kujua kitu mpaka uwe mjumbe wa Kamati Kuu?

**Panya:** Kwa hiyo, ulipewa muktasari na kuelezwa hayo yote? Ni nani aliyekuita?

**Lwaitama:** Chama kina watendaji wa chama, anaitwa Mashuve, Mndeme, ndio waliniita wakanieleza na nikajiridhisha kwa nyaraka nikatia saini.

**Panya:** Wakati unaitwa ulikuwa na mtu mwingine kuelezwa hayo? Ulikuwa peke yako au ulikuwa na wakili wako?

**Lwaitama:** Nilikuwa peke yangu, niliitwa nikaenda ofisini.

**Panya:** Hawa waleta maombi 19 walivyoitwa na Kamati Kuu walijibu wito na kutoa sababu kuwa wapewe nafasi, hii unaizungumziaje?

**Lwaitama:** Hiyo ninaikataa. Kwa mfano, mimi nimeitwa kuja hapa, nikatoka Moshi na kutii kufika, wao walishindwa hata mmoja wao kufika?

**Panya:** Umewahi kuona barua hiyo ya waleta maombi wakiomba Kamati Kuu kuwapa muda kidogo wa kufika mbele yake?

**Lwaitama:** Sababu niliziona na walisema sababu ya kwanza ni usalama na chama kiliwajibu.

**Panya:** (Anasoma barua mojawapo ya mleta maombi ya kuomba kuongezwa muda) Hizi sababu unazizungumziaje?

**Lwaitama:** Kwa kweli sababu ya kwanza ya kuwa wapewe muda wa kutafakari juu ya chama chao ninaichukulia ni kama walishindwa kukitazama chama kwanza kwa kuwa watu walikuwa kwenye taharuki ya chama, hivyo walipaswa kufika kutoa ufafanuzi wa hilo.

Inatia shaka wao kushindwa kufika kwa sababu hata hawakutuma wakili, yaani hii inatia shaka wote kushindwa kufika halafu wanasema wanakipenda chama.

Kwa sababu kama wanakipenda chama na chama kilikuwa kinawaka moto kwa kipindi hicho kutokana na kuwapo makundi na wao bado hawakutokea kwa ajili ya kutoa majibu ambayo watu walitamani kuyasikia.

Kuna wengine walitoka gerezani usiku, hapo ukiangalia Magereza, Usalama wa Taifa na polisi walihusika. Kwa hiyo, watu walitaka kujua 'ilikuwaje waliapishwa?'

Hivi hata kama walipata matishio ya usalama wao kuwa kuna watu wataandamana, tufikirie tu enzi za Rais Dk. John Magufuli kuna mtu anaweza kufanya maandamano au ilikuwa janjajanja yao tu!

**Panya:** Kuhusu usalama, Mbowe, Lissu na Lema waliondoka nchini.

**Jaji:** Mkiendelea hivi, nitatoa mwongozo wa maswali kwa sababu nimewapa uhuru mnautumia vibaya.

**Panya:** Baada ya kuona hicho kielelezo HDM 8, video, bado unataka kusema huyo ndio mwenyekiti aliyekuwa anataka akawasamehe?

**Lwaitama:** Kabisa.

**Panya:** Wabunge 19 malalamiko yao ni kwa viongozi wakuu wa chama na wakiwamo wapigakura, Mwenyekiti Mbowe alikuwa ni mmoja wa wapiga kura?

**Lwaitama:** Ni sahihi alikuwa ni miongoni

**Panya:** Kwa sababu ulipata bahati ya kuwapo kwenye kwenye Baraza Kuu na kura ilikuwa ya wazi, mwenyekiti alipiga kura gani?

**Lwaitama:** Kwa kuwa kura zilikuwa zinapigwa kwa makundi kwa kanda na nilikuwa tu ninaona watu wanasimama kwa kundi, sikuweza kuona kila mmoja mmoja kuwa nani alipiga ipi au ipi

**Panya:** Unakumbuka matokeo ya kura?

**Lwaitama:** Ndiyo na nimeyaandika

**Panya:** Matokeo yakoje? Nisomee hapo.

**Lwaitama:** Jumla ya waliopinga na wasiokuwa na upande ni watano sawa na asilimia 1.2, wasiokubalina na Kamati Kuu ni watano sawa na asilimia 1.2, waliokubalina na uamuzi wa Kamati Kuu 413.

**Panya:** Kwa hiyo Mbowe alipiga kura gani?

**Lwaitama:** Ukiangalia kwenye Kamati Kuu wajumbe wote walipiga kura ya kuunga mkono uamuzi wa awali

**Panya:** Kwa hiyo, walipewa nafasi ya kujitetea?

**Lwaitama:** Walipewa nafasi ya kujitetea kwenye Baraza Kuu

**Panya:** Kwa njia gani?

**Lwaitama:** Walipewa nafasi kwa njia ya maandishi na baadaye wakaulizwa iwapo wana cha kusema wakakaa kimya

**Panya:** Waliokuwa wanathibitisha nakala kama ni zao, ni nani alithibisha kuwa zile zilikuwa sawa na zile za wajumbe?

**Jaji:** Uliza swali lingine hilo siyo swali

**Panya:** Kura zilipokuwa zinapigwa ni kwanini zilipigwa kwa wanaokubaliana na uamuzi wa Kamati Kuu na kwanini ilisomeka kuwa wanaopinga uamuzi? Kwanini usiseme kuwa wanaokubaliana na warufani?

**Lwaitama:** Maswali yalikuwa matatu na yalikuwa ni wanaopinga au wanaokubaliana na wasiounga mkono upande wowote.

**Panya:** Je, warufani walipewa nafasi ya kutoa maneno ya hitimisho?

**Lwaitama:** Walihitimisha kwa njia za maandishi.

Baada ya maswali hayo, upande wa wajibu maombi, ukiongozwa na Wakili Peter Kibatala, ukamtaka Dk. Lwaitama kueleza jinsi Mdee na wenzake walivyoitwa mbele ya Baraza Kuu na majibu waliyoyatoa.

Kesi iliahirishwa hadi Aprili 18 na 19 mwaka huu, upande wa waleta maombi utakapomwuliza maswali ya dodoso mjumbe Lucy Mollel.

HABARI KITAIFA

# Mkurugenzi apongeza mgodi kufungua fursa kwa wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Zahara Michuzi ameipongeza Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kuanzisha programu zinazolenga kufungua fursa mbalimbali zinazowainua wanawake kielimu, kijamii na kiuchumi.

Pia ameipongeza kampuni hiyo kwa kuendelea kujali wananchi wanaozunguka mgodi huo kupitia mpango wa uwajibikaji wa kampuni kwa jamii (CSR) pamoja na kutekelezwa matakwa ya Sheria Madini kiasi cha kuwa mshindi mara mbili katika tuzo za Mlipakodi Mkubwa wa Sekta ya Madini.

Zahara alitoa pongezi hizo juzi wakati wa mzungumzo yake na waandishi wa habari mjini Geita kuhusu Siku ya Wanawake Duniani.

Alisema GGML na halmashauri hiyo wamekuwa wakishirikiana vizuri katika programu za kuwajengea uwezo wasichana kupitia shule wanazosoma.

Alitolea mfano mwaka jana walitoa mafunzo maalum kwa wanafunzi wa Shule ya Wasichana Nyankumbu ya mkoani hapa.

"Mwaka huu tutafanya kwenye shule nyingine ambapo tutakusanya wasichana wa shule za sekondari na msingi ili kuwahasisha kuona namna gani wanawake tuna nafasi sawa na wanaume katika kutimiza malengo ya taifa zima," alisema.

Pamoja na ushirikiano huu, aliwataka wadau wa mkoa huo kuwa mfano wa kuigwa kama GGML ambao wamekuwa wadau wazuri kiasi cha kushinda tuzo kila mwaka, ikiwamo ya Mlipakodi Bora.

"Ina maana GGML inaunga mkono serikali kutoa huduma bila kuwa na vikwazo vya kibajeti. Kwa hiyo, ushirikiano unahitajika na sisi tulioaminiwa kwa niaba ya serikali tutawapa ushirikiano wa kutosha kuhakikisha lengo na adhma ya serikali kutatua changamoto za wananchi linafikiwa," alisema.

Akizungumzia Siku ya Mwanamke Duniani, Zahara alisema ni siku ambayo inamkumbusha wanawake nao wana uwezo sawa na jinsia nyingine.

"Nimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutambua na kuamini katika jinsia ya kike hususani sisi tulio katika umri mdogo, kulinganisha na dhana iliyokuwapo hapo zamani kwani kwa umri wetu usingeteuliwa kupewa majukumu makubwa.

"Lakini pia tunashukuru kwa imani yake kwetu imetufanya tujiamini na kujituma kumwaminisha kuwa hakututeua kwa bahati mbaya wala kufanya makosa kwa sababu tuna uwezo, nia na nguvu sawa na wanaume waliokuwa wakiaminiwa zamani.

"Niwasihi viongozi wengine wendelee pia kuamini wasichana na wanawake wenye uwezo katika maeneo wanayowaongoza ili kuwainua na kuwaaminisha kuwa wanaweza kufanya makubwa zaidi ya sisi tulioaminiwa sasa," alisema.

Aliwashauri mabinti wadogo na wanawake wenzake wajiamini kuwa wanaweza, waamini kipawa walichopewa na Mungu na wasijidharau hata wanapopitia misukosuko ya kurudishwa nyuma, waseme ili kumsaidia mwingine aliyekwama ainuke na kusaidiwa kwa sababu taasisi zipo nyingi, kuanzia serikali na taasisi binafsi.

Alitoa wito kwa wanawake kutoa vipawa walivyonavyo wasivifiche, kwa sababu serikali ipo kuwaunga mkono ikiwa ni pamoja na GGML kuhakikisha mwanamke harudishwi nyuma ili waende kwenye usawa ambao wanaupigania kwa sasa.

GGML imekuwa ikitekeleza programu mbalimbali za kuwainua wanawake ikiwamo programu ya Female Future Tanzania Programme (FFT) ambayo inaratibiwa na Chama cha Waajiriwa Tanzania (ATE) kwa lengo la kuwajengea uwezo wanawake kushika nyadhifa za juu.

Pia kampuni hiyo ambayo hutoa kipaumbele cha ajira kwa wanawake, inatekeleza programu ya masomo ya shahada ya uzamili katika usimamizi wa biashara (MBA) pamoja na programu nyingine za mafunzo ndani ya kampuni kwa lengo la kuwainua wanawake kushika nafasi za juu za uongozi.



Dk. Tijo Xaver wa Hospitali ya Regency ya jijini Dar es Salaam, akimpima mmoja wa wagonjwa, wakati wa kambi ya kupima figo bure iliyoandaliwa na hospitali hiyo, kuadhimisha Siku ya Figo Duniani juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# ACT: Tuchukue hatua kukabili njaa

**Na Julieth Mkireri,** KILWA

CHAMA cha ACT Wazalendo kimeitaka serikali kuchukua hatua dhidi ya upungufu wa chakula kwa kuhakikisha inapanga bei za vyakula, kikidai kuwapo baadhi ya familia zinazopata mlo mmoja kwa siku.

Makamu Mwenyekiti Bara wa chama hicho, Dorothy Semu alitoa rai hiyo jana wilayani Kilwa mkoani Lindi alipozungumza katika mkutano wao wa kisiasa.

Alisema serikali haijaleta ufumbuzi wa suala hilo, hali inayowaumiza wananchi wenye vipato vidogo.

Semu alisema zipo familia ambazo zinakula mlo mmoja kwa siku na wengine miwili kutokana na kukosa fedha kwa ajili ya kununua chakula.

"Serikali ilisema imeagiza chakula nje, isimamie kiingie sokoni kunusuru wananchi na kupanda kwa bei. Tunaitaka serikali iachie chakula kilichopo kwenye maghala kutokana na hali kuwa ngumu na wananchi kusumbuliwa na uhaba wa chakula," alisema.

Pia alisema wakulima wanatakiwa kuwezeshwa kufanya kilimo cha kisasa na kupata pembejeo kwa gharama nafuu ili kuzalisha kwa wingi.

"Serikali inatakiwa kuwawezesha wakulima kutoka katika kilimo cha msimu na kufanya kilimo cha umwagiliaji ili walime mwaka mzima na wajengewe uwezo wa kuhifadhi chakula cha kutosha kupitia mradi wa kitaifa (Mamlaka ya Uhifadhi wa Chakula NFRA)," alisema.

Mwenyekiti wa chama hicho, Juma Duni Haji alisema ili kuwe na mabadiliko yanayokua kwa kasi, ni lazima wananchi waseme vikwazo vyao kwa sababu Rais Samia Suluhu Hassan yupo kwa ajili ya kuleta ahueni na kuleta mabadiliko.

Kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe alisema ili kuwa na maendeleo, ni lazima kuwa na nchi inayofuata misingi ya utawala wa sheria kwa kutoa haki kwa wote bila ubaguzi.

Zitto alidai wapo watu hawajulikani walipo na wapo wavuvi waliathiriwa kwa nyavu zao kuchomwa moto na kuitaka serikali ifanye uchunguzi kuhusiana na matukio hayo na hatua za kisheria zichukuliwe.

"Hatuwezi kuendelea kulalamika tena, tunachotaka uchunguzi ufanyike ijulikane watu hawa wako wapi? Hatuwezi kuponya taifa kama hatuwezi kusema ukweli," alisema.

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**SILADJI MUNYANDINDA ATHUMANI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T. 191 DLJ aina ya **TOYOTA HIACE**, yenye Chassis No. **RZH1254012836**, Engine No. **2RZ3125541**, Engine Capacity **No. 2430.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya Polisi. **KAH/RB/181/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZA MJINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 464 YA MWAKA 2022**
**CHARLES MICHAEL TEFFE..........MDAI**
**DHIDI YA**
**MMG LIMITED......MDAIWA**
**KUITWA SHAURINI**

MAHAKAMA HII INAKUFAHAMISHA KWAMBA MDAI AMEFUNGUA MADAI DHIDI YAKO.
SHAURI LIMEPANGWA KUSIKILIZWA MNAMO TAREHE 14/03/2023 SAA 2:00 ASUBUHI KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI NA UNATAKIWA KUWEPO, AU KUWAKILISHWA KISHERIA PAMOJA NA KULETA UTETEZI WAKO DHIDI YA MAOMBI HAYA.
ZINGATIA KWAMBA KUTOKUFIKA KWAKO TAREHE HIYO, SHAURI LITAANZA KUSIKLIZWA BILA WEWE KUTAARIFIWA TENA, NA MAAMUZI KUTOLEWA.

**HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI**
**MAHAKAMA YA MWANZA MJINI**
**MWANZA**

KINAMAMA WANAPOJIVUNIA WIKI YAO...

# Chombo cha kinamama wasomi nchini kilichobeba dhamira kuvusha jinsia yao

## • Mwanzilishi Mwenza, mgeni mwenye nusu karne nchini

**Na Christina Mwakangale**

KILA penye mafanikio, daima mzizi wake ni penye wazo na kisha mikakati ya utekelezaji ikachukua nafasi yake, ikiwamo upatikanaji rasilimali za watu na fedha.

Rasilimali fedha inafahamika kuwa nyenzo muhimu, ili kukamilisha malengo ya wazo hilo, kwa kuwa hufungua njia na mipango ya utekelezaji.

Ndivyo mwanaharakati, Mary Rusimbi, alivyokuwa na ndoto ya kufanikisha kuwainua wanawake wenzake, kupitia vikundi, asasi, mashirika waliojiunga pamoja kutekeleza malengo yanayofanana, wote kumkwamua mwanamke.

Pamoja na ndoto yake kufanikiwa kwa kuanzisha Mfuko wa Udhamini wa Wanawake Tanzania (WFT-T) mwaka 2008 na kuzifikia asasi takribani 400, anasema anatazamia miaka 50 ijayo uwezeshaji uongezeke.

"Nilipata wazo mapema, ila namna ya kuliunganisha na likafanikiwa ilichukua miaka. Nilikutana na mwanzilishi mwenzangu (Marije Te Riele), wakati huo nipo ubalozini tukaja na kitu kimoja.

"Mfuko huu ulikuwa wazi na filosofia na tulijiweka wazi kwamba ni watu wa kifeminia, wanaharakati wa kutafuta ufadhili kwa ajili ya kuwezesha wanawake kuondokana na ukatili wa aina yeyote," anasema Mary.

Mary, Mwanzilishi Mwenza wa Mfuko huo, anasimulia namna ulivyoanza na kulikuza wao hilo, akisema: "Nilikutana na mzungu mmoja akaniambia nasikia Mary unastaafu nikamjibu nafungua mfuko wa wanawake akasema sawa chukua dola 100."

Wakati akianza kuwezesha asasi tofauti, Mary anasema mfuko huo kwa mwaka ulianza kwa kutoa ruzuku tatu mwaka 2011 na zikatolewa 67 mwaka 2020, huku zikipungua na kufikia 48 msimu wa Uviko-19.

"Ndoto yangu imetimia tulijua matokeo hayatakua leo leo, fikiria bila fedha, tupo wawili, ukifikiria ni uthubutu tu. Ndoto yangu mfuko uishi miaka 50 zaidi na ajenda iwe endelevu," anasema Mary.

"Kwa bara la Afrika ni mfuko wa tano wenye dhamira hiyo hiyo ya kuwezesha wanawake na wasichana kupambana na mifumo kandamizi, ili kuwezesha ukombozi wao kimapinduzi.



Marije Te Riele (kushoto) akimlisha keki Mwanzilishi Mwenza, Mary Rusimbi, kuadhimisha miaka 15 tangu waanzishe Mfuko wa Udhamini wa Wanawake Tanzania (WFT-T), kwenye maadhimisho yaliyofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM). **PICHA ZOTE: CHRISTINA MWAKANGALE.**

"Mfuko huu ni sehemu ya mtandao wa mifuko takribani 44, katika dunia yenye dhamira ya kuwezesha wanawake kujikomboa kiuchumi, kifikra, na kijamii," anasema.

Pia, anasema malengo ya mifuko hiyo inayofanana na shughuli zake, ni kuchochea mabadiliko ya kimapinduzi katika kupambana na mifumo kandamizi inayowawekea vikwazo vya kufikia, kutumia na kunufaika na rasilimali za taifa lao.

"Takribani asilimia 60 ya ruzuku zinaelekezwa katika ngazi ya jamii ili vikundi vya wanawake katika ngazi hii, kuendeleza vuguvugu la utetezi wa haki zao, kiuchumi, kijamii na kisiasa," anasema Mary.

**MWANZILISHI MWENZA**

Marije Te Riele, mwanzilishi mwenza wa chombo hicho, anasema alipofika barani Afrika, alikuwa binti mdogo wa umri wa miaka 21 na sasa na ametimiza miaka 71 akifanikwa kuanzisha mfuko huo na mwenzake, Mary.

"Pamoja na kazi nyingi ubalozini (Uholanzi-nchini), niliweza kukutana na Mary na tukaunganisha ndoto zetu. Ndoto inakuwa na maono, lakini hadi sasa nina imani mfuko upo mikono salama na tuyatarajiayo," anasema Marijie.

Anasimulia kwa kipindi cha miaka 15, mfuko umejiimarisha kitaasisi na wakijivunia matunda ya kazi pamoja na kuibua mjadala kuhusu mifumo ya utoaji rasimilimali na ruzuku, ambazo haziwafikii walengwa hususan wanawake na wasichana.

**WADAU WAUNGA MKONO**

Baada ya mfuko huo kuzaliwa rasmi, wadau waliojitokeza kuunga mkono nia ya waanzilishi hao pamoja asasi watekelezaji wa miradi kutokana na ruzuku, wana mengi ya kusema, akiwamo Shamshad Rehmatullah, muungaji mkono wa awali.

Anasema mara baada ya mfuko huo kuundwa tayari alikuwa mwanaharakati, mtetezi wa haki za wanawake, akisema akiwa kwenye kazi zake za uwakili alikutana na mengi kuhusu masuala ya kundi hilo.

"Mimi nilikuwa mwalimu wa Chuo cha Ushirika Moshi na kama mwanasheria niliona mengi, nikiona mwanamke anakosa haki, ardhi na niliona mengi nikiwa wakili, haja ya 'ku-support' (kuunga mkono) mfuko kama huu.

"2010 wakati wa mchakato wa katiba ukianza nilikuwa mwanaharakati wa kutetea wanawake, wapo waliofika kuomba ruzuku kwenye taasisi, walikuwa wanaume na wana maandiko kuhusu wanaume, niliwahi kutoa ruzuku TAWLA (Chama cja Waandushi wa Habari Wanawake), wakati huo nikiwa na ofisi n dogo tu.

"Wakaja UN Women (Waandishi wa Habari wa Umoja Mataifa), kunihoji tena kwenye ofisi ndogo tu. Nasema ukiwa mwanamke na katika taasisi makini na kutaka kutimiza lengo, inasaidia wengi," anasema Shamshad.

Kwa tafsiri ya kipekee, mwanaharakati anasema tangu akiwa binti, Chuo Kiku cha Dar es Salaam (UDSM) Ave-Maria Semakafu, hivi sasa ni msommwenye elimu ngazi ya shahada ya uzamili, anasema alijiona kuwa upande wa harakati za utetezi siku nyingi.

"Miaka 24 tu nimeanza harakati wakati huo kukiwa na Chama cha Wanataaluma Wanawake (IDS) nimelelewa humo, nilipomaliza na wakati wa maandalizi ya Beijing, tuliandaa kitaifa, kupata sauti za wanawake," anasema Dk. Ave-Maria.

"Baadae maandalizi yakapanda kikanda, Afrika Masharikі kishaa tukaenda Dakar (Senegal) ajenda moja ya Afrika," anasema.

Kwa uwakilishi kutoka barani Afrika Kwenda Beijing, China, Dk. Ave-Maria anasema walifikia 360 na kwamba wanawake hao waliporejea nchini mwao, utekelezaji na mabadiliko ya kutetyea masuala ya wanawake yalishamiri.

"Baada ya uchaguzi mkuu 2015 kila mtu naona anataka kutoka na lake kuonekana yuko tofauti. Tunatakiwa kuwa na nguvu ya pamoja na kuindeleza.

"WFT-T akiwa mwezeshaji na mratibu wa kutoa ruzuku, tunashukuru kupitia kwao tuliwafikia wanawake wengi, lakini ruzuku isitutenganishe na ajenda zetu tuwe kitu kimoja," anasema Dk. Ave-Maria, Mratibu wa Kitaifa wa Taasisi ya Wanawake ya Ulingo (TWCP).

WAJIKI

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza, kati ya asasi zilizofikiwa na mfuko huo, anasema shirika lilipata ruzuku kutoka WFT-T ya Sh. milioni 80, kwa ajili ya kampeni mwaka 2022/23.

Kampeni lengo lake, linalotajwa na mkurugenzi huyo ni kunusuru wanafunzi dhidi ya rushwa ya ngono, akisema ni moja ya kikwazo kikubwa kinachosababisha, baadhi ya wanafunzi kushindwa kutimiza ndoto zao.

Janeth anafafanua kwamba, shuleni na vyuoni, mitaani pia wanakumbana na kikwazo kama hicho kutoka kwa madereva wa bodaboda, bajaji na hata daladala, kuwashawishi kwa lifti.

"Awamu ya kwanza hadi ya nne ya kampeni, tumefikia madereva 3,742 na shule 24 na ya tano tumepanga kufikia kata 18, kwa kila wilaya kata sita kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa ya ngono," anasema.



Washiriki wa maadhimisho hayo wakisheherekea.



Meneja Mawasiliano na Mahusiano wa kampuni ya Sukari Kilombero, Willa Haonga (kushoto), akikabidhi zawadi za washiriki kwa Mkuu wa Idara ya Rasilimali Watu, Diana Mwakitwange, wakati wakiadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Kilombero, mkoani Morogoro mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwanakijiji alalama majibu DNA kucheleweshwa na polisi

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

MKAZI wa Kipondoda, Kata ya Manyoni wilayani Manyoni, Vicent Kayegele amemwomba Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba aingilie kati na kusaidia kutolewa majibu ya vipimo vya vinasaba (DNA) vya mtoto wake aliyeuawa miaka miwili iliyopita.

Amesema kuna haja majibu ya vipimo hivyo yatolewe na mamlaka husika ili awe na uhakika kama mwili aliouzika ni wa mwanawe au la.

Akizungumza juzi wakati Mkuu wa Mkoa wa Singida, Serukamba, anapokea kero kwa wananchi wa Wilaya ya Manyoni, mwanakijiji huyo alisema mtoto wake aitwaye Neema Vicent anadaiwa kuuawa na mumewe Aprili 30, 2020 eneo ka Tambukareli, Kata ya Manyoni na mwili kuufukia mita chache kutoka kwenye nyumba yao.

Alisema kuwa baada ya tukio hilo kutokea, mtuhumiwa wa mauaji alikimbilia kusikojulikana na kwamba mwili wa marehemu uligundulika baada ya siku 45 ukiwa umefukiwa kwenye shimo, hivyo kuharibika.

Kayegele alisimulia kuwa baadaye askari watano walifika katika eneo ulikofukiwa mwili wa marehemu ambapo waliuchukua na kuupeleka mochwari ya Hospitali ya Wilaya ya Manyoni kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Alisema kuwa mwili ukiwa mochwari, askari walimwagiza mhudumu wa mochwari kutoa mifupa miwili ya videole vya miguu, kucha tatu za mkononi, nywele na meno mawili kwa madai wanakwenda kuvifanyia uchunguzi wa vinasaba (DNA) kubaini kama mwanamke huyo aliyeuawa ni mtoto halali wa Vicent Kayegele.

Mwanakijiji huyo alisema kilichowashangaza kama familia ni kitendo cha askari hao kutochukuliwa vipimo vyovyote vya mzazi mmoja wapo mama au baba na hadi sasa toka Juni 16, 2020, viungo hivyo vilipochukuliwa ikiwa ni zaidi ya miaka miwili hakuna majibu yaliyotolewa, hali ambayo inatia shaka utendaji kazi wa Jeshi la Polisi.

Aliongeza kuwa amejitahidi kuwasiliana na ofisi kadhaa za serikali ili kusaidiwa kupata majibu ya DNA ya mtoto wake ikiwamo kuandika barua Aprili 29, 2021 kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora lakini hadi sasa hakuna majibu yoyote, jambo lililomfanya aanze kukosa imani ya serikali.

"Ninachokiomba majibu ya DNA yatolewe ili niwe na uhakika mwili niliouzika ni mtoto wangu kweli, maana siku tunauchukua ulikuwa umeharibika, hivyo ilikuwa sio rahisi kuutambua," alisema.

Kufuatia hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Serukamba, alimwagiza Mkuu wa Polisi Wilaya ya Manyoni (OCD) kufuatilia suala hilo na kuhakikisha majibu ya vipimo vya DNA yanatoka.

# Chuo cha Maji chatakiwa kuongeza ubunifu kikazi

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amekisisitiza Chuo cha Maji kujiimarisha katika ubunifu kiwe na maabara ya kufanya utafiti na kutoa majibu ya changamoto zinazoikabili sekta hiyo.

Waziri Aweso aliyasema hayo juzi mkoani Dar es Saalam alipofungua kongamano la kimataifa la kisayansi lililoratibiwa na Chuo cha Maji kwa kushirikiana na wizara husika.

Alisema lengo la Rais Samia Suluhu Hassan ni kumtua mama ndoo ya maji kichwani na kuleta maendeleo zaidi kwa jamii.

"Kongamano hili ni moja ya tukio la wiki ya maji hivyo kuweni na maabara ya kutoa majibu katika sekta ya maji, kwasababu serikali imewekeza fedha nyingi katika miradi mbalimbali ya maji inayotekelezwa hapa nchini," alisema Aweso.

Aliongeza kuwa teknolojia na mazingira vinabadilika hivyo ni muhimu kubadilika na kwenda na wakati, akisisitiza kwamba mabadiliko yanahitaji wataalamu zaidi katika kuendesha na kusimamia miradi ya maji.

Aidha, alieleza kuwa kufanyika kwa kongamano hilo kwa mara ya pili ni moja ya njia ya kubadilishana uzoefu na mbinu kutoka nchi mbalimbali, ili kuimarisha huduma ya maji nchini.

Naye Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Cyprian Luhemeja, alisema siku za usoni kongamano hilo litaimarishwa zaidi kisekta, lengo likiwa kuweka mikakati ya kufikisha na kuimarisha huduma ya maji katika jamii.

Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Adam Karia, alisema wadau zaidi ya 500 kutoka ndani na nje ya nchi wanashiriki kongamano hilo linalofanyika kwa mara ya pili nchini.

Kongamano la kimataifa la kisayansi la maji ni moja ya matukio ya wiki ya maji ambayo rasmi ilianza kuadhimishwa nchini mwaka 1988, ikiwa na matukio mbalimbali kuelekea Siku ya Maji Duniani inayotarajiwa kufanyika Machi 22, mwaka huu.

# Wauguzi mbaroni tuhuma kuwauzia dawa wagonjwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAUGUZI saba kwenye Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za wizi wa dawa na kudaiwa kuwauzia wagonjwa nyakati za usiku.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Anderson Msumba, aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema kwa muda mrefu amekuwa akipokea malalamiko ya wagonjwa ya kuuziwa dawa usiku wa manane na wauguzi kinyume na sheria za utumishi wa umma.

Alisema baada ya kupokea malalamiko hayo waliyafanyia kazi kwa kushirikiana na maaofisa kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya na Februari 24, mwaka huu, walifanya ukaguzi wa kushtukiza katika hospitali.

Msumba alisema katika ukaguzi uliofanyika kwa wauguzi wa zamu siku hiyo, saba walikutwa na dawa kwenye mikoba yao ya mikononi pamoja na dripu za maji.

Alisema wauguzi hao walikamatwa na kufikishwa katika kituo cha polisi kwa ajili ya mahojiano.

"Dawa wanazouziwa wagonjwa wetu hospitalini na wauguzi hawa hatujui ubora wake na wapi wanazitoa, kwasababu biashara hiyo wamekuwa wakiifanya usiku wa manane katika wodi na hii inasababisha hospitali kukosa mapato yake vile inavyotakiwa,"alisema Msumba.

Aidha, alisema baada ya tukio hilo alifanya kikao kazi na wauguzi wa hospitali hiyo na kukubaliana kutumika geti moja la wagonjwa wa nje kwa sababu awali yalikuwa yakitumika mageti mawili.

Pili walikubaliana kila siku msimamizi wa wodi kutoa taarifa yake ya kila siku.

Hata hivyo Msumba alisema, uchunguzi wa Jeshi la Polisi utakapokamilika watachukua hatua zingine za kiutumishi, huku akiwataka watumishi wa kada ya afya kuacha tabia ya kuuza dawa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kocha mpya Stars apewe muda ili kufikia malengo

**SERIKALI** kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, imemtambulisha Kocha mpya atakayeinoa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Adel Amrouche, ambaye ana uraia pacha wa Algeria na Ubelgiji.

Amrouche ametua Tanzania akitokea Yemen, ambapo alikuwa akiifundisha timu ya taifa hilo, ingawa kadumu kwa muda mfupi kwenye nchi hiyo.

Kocha huyo amewahi kufundisha timu za Taifa mbalimbali ikiwamo Burundi, Libya, Botswana, Equatorial Guinea na Kenya maarufu kwa jina la Harambee Stars ambayo aliweka rekodi ya kucheza mechi 20 bila kufungwa.

Lakini pia kocha huyo ana uzoefu wa kufundisha klabu mbalimbali za Afrika ikiwamo USM Alger ya Algeria huku akiiongoza kwa mafanikio zaidi DC Motema Pembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Rasmi ametua Tanzania na kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Wilfred Kidao, kocha huyo amepewa mkataba wa miaka mitatu na msaidizi wake ni Hemed Suleiman 'Morocco' kutoka Zanzibar.

Kwanza kabisa tunapenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kumleta kocha huyo na kuweka wazi wao ndio watamlipa mshahara mwalimu huyo. Pia imeweka wazi imeanza na mchezo wa soka, michezo mingine itafuata kwa ajili ya kuhakikisha timu zote za taifa zinakuwa na makocha wenye uzoefu wa kutimiza malengo.

Haya ni mapinduzi mengine ambayo yamefanywa na uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, yanatakiwa kupongezwa na kupewa heshima ya kufanya vizuri katika kila mashindano ambayo Taifa Stars itashiriki.

Rais Samia ameonyesha mapinduzi makubwa kwa kushiriki kuanzia kwenye maandalizi na si kusubiri kupata matunda ya ushindi kama ambavyo sasa ameongeza hamasa ya kununua mabao yanayofungwa na wachezaji wa Simba na Yanga, zinazoshiriki michuano ya kimataifa.

Baada ya kufahamu hilo, ni vyema viongozi wetu wa TFF na timu ambazo zinaishi na wachezaji kwa muda mrefu kumpa ushirikiano kocha huyu ili atimize majukumu yake vizuri na si kukumbana na changamoto yoyote.

Kocha anapohitaji kukutana na wachezaji, viongozi wa timu kwa kushirikiana na makocha wanatakiwa kuheshimu kwa kutoa ruhusa mapema, tunaamini kocha huyo na TFF watafanya kazi zao kwa kuheshimu taratibu za Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA) na zile za Shirikisho la Soka Afrika (CAF).Ili Amrouche atupatie Watanzania matunda mazuri, ni lazima apewe ushirikiano wa dhati na wadau wote, kocha anapopata ushirikiano na kupewa mahitaji yake kikamilifu, uwezekano wa Taifa Stars kupata matokeo chanya huwa mkubwa.

Kila mmoja kutokana na nafasi husika aliyonayo akitekeleza majukumu yake vizuri, Taifa Stars yenye makali na ile iliyokuwa tishio katika miaka ya 1980 itarejea.

Ikumbukwe mafanikio yoyote hayapatikani kwa njia ya mkato au miujiza, maandalizi sahihi na uwajibikaji wa kila Mtanzania utatupeleka kule walipo Afrika Magharibi na Kaskazini, na si vinginevyo.


Amrouche baada ya kutambulishwa aliweka wazi ili afikie ndoto za Watanzania, anahitaji ushirikiano mkubwa wa mashabiki wa soka kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini, anaamini ushirikiano ndio silaha namna moja itakayofanya kazi yake kukinoa kikosi hicho kuwa rahisi.

Mkufunzi huyo wa kimataifa alisema anaamini mashabiki wana nafasi kubwa katika kuipa maendeleo Taifa Stars na si kuwatisha wapinzani pale timu hiyo inapokuwa uwanjani, kwa sababu huwaongezea nguvu wachezaji.

Mwalimu huyo pia ameweka wazi anapenda zaidi kuwapa nafasi vijana kwa sababu anaamini ukiwekeza kwa wachezaji chipukizi, umewekeza katika hazina ya muda mrefu, hivyo ni wakati mwingine kwa wachezaji wenye umri mdogo kujiandaa kuitumikia nchi katika mashindano mbalimbali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera Simba, Yanga kuliheshimisha Taifa

Na Adam Fungamwango

**KWA** mara ya kwanza, klabu kongwe nchini Tanzania, Simba na Yanga zimepata ushindi kwa pamoja zikicheza kwenye viwanja vya nyumbani, mechi za kimataifa.

Haijawahi kutokea kwenye historia ya soka Tanzania timu hizo zote kuwa kwenye michuano ya kimataifa ngazi ya makundi, haijalishi Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho.

Kwa sababu huko nyuma Tanzania ilikuwa inapeleka timu moja tu kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, na moja nyingine Kombe la Shirikisho.

Tangu Simba ilipocheza mara mbili michuano ya Ligi ya Mabingwa, Tanzania ilivuna pointi nyingi na kusababisha kwa mara ya kwanza kuingiza timu nne.

Mbili zinacheza Ligi ya Mabingwa na mbili Kombe la Shirikisho. Hata Simba na Yanga ambazo zinacheza michuano ya kimataifa, zote zilikuwa Ligi ya Mabingwa, na zile mbili zilizokuwepo Kombe la Shirikisho, Azam na Geita Gold zilitupwa nje.

Kwa pointi jinsi zilivyo, ni kwamba msimu huu timu yoyote ile kati ya mbili, ikifanikiwa kumaliza ikiwa ya tatu kwenye kundi, basi msimu ujao bila kuangalia matokeo au pointi za timu za nchi zinazoyemelea nafasi hiyo, Tanzania itapeleka tena timu nne kwa mara nyingine tena.

Na kwa matokeo ya mechi za Jumanne na Jumatano iliyopita wala sipati shaka kusema nafasi hiyo itapatikana kwa msimu ujao.

Kwa sababu si tu kwamba Simba na Yanga zote zinaweza kumaliza nafasi ya tatu kwenye makundi hayo, bali hata kwenda hatua ya robo fainali.

Na kama itakuwa hivyo itakuwa pia inajiwekea akiba pointi zingine za misimu mingine.

Jumanne iliyopita, Simba iliichapa Vipers bao 1-0, mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba inayoshika nafasi ya pili sasa kwenye Kundi C, kutinga kwao robo kuko mikononi mwao kama itapata ushindi wowote ule kutoka kwa Horoya, mechi inayotarajiwa kuchezwa Machi 17, Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Timu hiyo kwa sasa ina pointi sita, Horoya ikiwa na pointi nne, hivyo kama ikipata ushindi itafikisha jumla ya pointi tisa, ambazo timu hiyo ya Guinea haiwezi kuzifikia hata kama itaifunga Vipers kwenye mechi ya mwisho, ambapo itafikisha pointi saba tu.

Kwenye kundi hilo, tayari Raja Casablanca ambao ndiyo vinara wakiwa na pointi 12, wameshafuzu.

Yanga ambayo ipo kwenye Kombe la Shirikisho, kwenye Kundi D, nayo kama Simba ipo nafasi ya pili, ikiwa na pointi saba chini ya vinara Monastir ya Tunisia ambao tayari nayo imeshafuzu ikiwa na pointi 10. Kufuzu kwa Yanga nako kuko mikononi mwao kwani iwapo itashinda mechi yao ya Machi 18 kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa, dhidi ya Monastir kutaifanya timu hiyo kwenda moja kwa moja kwenye hatua inayofuata, kwani itafikisha pointi 10 ambazo TP Mazembe haiwezi kuzipata hata kama itashinda mechi zake zote mbili ilizosaliwa nazo.

Tayari timu hizo zimeshazoa jumla ya Sh. Milioni 40 zilizoahidiwa na Rais Samia, akitoa Sh. Milioni 5 kwa kila bao litakalopatikana kwa timu hizo.

Kwenye mgawanyo huo, Yanga imepata Sh. Milioni 30, zilizopatikana baada ya kuichapa TP Mazembe bao 3-1, sare ya bao 1-1 ugenini dhidi ya Real Bamako na mabao 2-0 dhidi ya timu hiyo hiyo ya nchini Mali jijini Dar es Salaam.

Simba mpaka sasa imejipatia Sh. Milioni 10, kwani ilishinda bao 1-0, mechi zote mbili za nyumbani, na haikupata kitu ilipochapwa mabao 3-0 nchini dhidi ya Raja Casablanca.

Tunatoa pongezi kwa timu hizo zote kwa kuliheshimisha taifa, kwani sasa hata kama kuna baadhi ya watu nje ya nchi walikuwa na wasiwasi na soka la Tanzania, basi watakuwa wameshakubali kuwa limepiga hatua kubwa sana.

Na wala tusipepese macho kuwa usajili wa idadi kubwa ya wachezaji kutoka nje ya nchi umesaidia sana timu za Tanzania kupiga hatua kwenye michuano ya kimataifa ngazi ya klabu.

Binafsi sidhani kama ingekuwa hivyo kama timu zingekuwa hazina wachezaji wa kigeni, au zingekuwa na ndogo tu. Hata ukiangalia mabao yote manane yaliyofungwa mpaka sasa, saba yamefungwa na wachezaji wa kigeni.

Kwa hili linaloonekana sasa, wala haishangazi tukiona wachezaji wengi wa kigeni wakizidi kumiminika kucheza soka Tanzania, ambapo zamani walikuwa wakikataa kwa sababu hakuziona klabu zikifanya vema kimataifa.

Kinachotakiwa sasa ni kwa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kuweka utaratibu mzuri kuboresha ligi ambapo itaendelea kutupatia wawakilishi bora na imara, pia kuweka mazingira rafiki kwa wachezaji wa kigeni kuendelea kuingia kuitangaza ligi na klabu zetu kimataifa.




Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, mkoani Mwanza, Wanchoke Chinchibera (wa nne kushoto), akikata utepe kuzindua duka la Vodacom, wilayani humo jana. Wengine ni Mkuu wa Vodacom Kanda ya Ziwa, Ezekiel Nungwi (wa nne kulia) na baadhi ya wafanyakazi wa kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Kamati, viongozi ZBS wazuru TBS kimkakati

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kilimo, Biashara na Utalii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar imeridhishwa na ushirikiano uliopo baina ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS), ikisisitiza uendelezwe kwa kuwa matunda yake yanaonekana kwa maslahi mapana ya pande zote mbili za Muungano.

Jijini Dar es Salaam juzi, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii, Yusuf Hassan Iddi alitoa kauli hiyo, kamati yake ilipotembelea ofisi za TBS ili kujifunza shughuli zinazofanywa na shirika hilo. Wengine waliokuwa kwenye ujumbe huo ulioongozwa na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omary Said Shaaban, mbali na wajumbe wa kamati hiyo, pia walikuwapo wajumbe wa Bodi ya ZBS na Mkurugenzi wa ZBS.

"Kwa kweli tumejifunza mambo mengi sana na tunashukuru TBS kwa kuwashika mkono wenzetu wa ZBS na sasa wanafanya kazi zao vizuri sana tofauti na awali.

"Tunawaomba ushirikiano huu mwendeleze ili tuweze kufaidi matunda ya ushirikiano huo," alisisitiza.

Alisema kuwa katika ziara hiyo, walitembelea ofisi za TBS zilizoko bandarini na kujionea utaratibu wa ukaguzi wa bidhaa kutoka nje ya nchi kupitia mfumo wa Pre-shipment Verification of Conformity (PVoC) na ule wa DI.

"Kwa kweli tumejifunza mambo mengi sana kwenye One Stop Center ya TBS na jinsi walivyounganisha mifumo yao kwa ajili ya ukaguzi na utoaji wa mizigo bandarini," alisema Yusuf.

Pia alisema walitembelea makao makuu ya shirika na walipata maelezo jinsi TBS inavyofanya kazi zake.

"Kwa kweli ninakushukuru sana Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Yusuf Ngenya kwani tumejifunza mambo mengi sana na mnafanya kazi nzuri sana," alisema.

Alimpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi kwa kuboresha utendaji wa ZBS ambapo karibu Sh. bilioni nane zimewekezwa kwenye taasisi hiyo kwa upande wa maabara ili kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa zinapimwa na kukidhi viwango vinavyotakiwa.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe alisema kuwa kupitia ziara hiyo, wageni hao wamejifunza kazi mbalimbali zinazofanywa na TBS kuanzia bandarini ambako unafanyika ukaguzi wa mizigo mbalimbali kutoka nje kwa kukagua kabla ya kusafirisha kuja (PVoC) kwa kupitia mawakala wa TBS, lakini pia bidhaa zinazokaguliwa ndani baada ya kufika kupitia mfumo wa DI ili kuhakikisha zinakuwa na ubora unaotakiwa.

Kigahe alisema wageni hao walifika makao makuu ya TBS na kujionea maabara zinazotumika kupima bidhaa mbalimbali.

"Kwa hiyo, sisi kama wizara tumefarijika kwa wenzetu kufika kututembelea kujifunza lakini zaidi kuimarisha ushirikiano katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwani tunahakikisha kwamba ushirikiano huo nchi wa kimuungano kwa faida ya nchi na taasisi zetu zinazofanya kazi pamoja," alisema Kigahe.

Alifafanua kwamba wawakilishi hao wakielewa vizuri taasisi hizo, maana yake watasaidia kuhakikisha wanatoa elimu kwa wazalishaji ili kuhakikisha wanafuata viwango vile ambavyo vinawekwa na mashirika hayo, pia walaji wataelewa namna ya kutambua bidhaa zenye viwango.

Alisema ushirikiano huo utawajengea msingi wa kuhakikisha wanaboresha bidhaa ili bidhaa zote ziwe na viwango vinavyowiana na kushindana kwenye soko la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

"Zaidi sasa tumeridhia mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika ambapo sasa tutashindana Afrika nzima, kwa maana bidhaa zinazotoka nchini zitatambulisha Tanzania na sio Zanzibar au Tanzania Bara.

"Kwa hiyo, mwelekeo huu tunakwenda kuwa na matokeo chanya kwenye upande wa uchumi wa nchi zetu," alisema.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omary Said Shaban alisema lengo la ziara hiyo ni kujifunza, kuongeza uelewa na kubadilishana uzoefu kwa TBS na ZBS ambazo zimekuwa na ushirikiano.

Alisema wameleta wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuwa wao ndiyo walitunga sheria iliyoanzisha ZBS na sasa imepita muda tangu sheria hiyo itungwe na ZBS ianze kazi, hivyo kufanya ziara kama hiyo kutoa fursa ya kujua taasisi waliyoianzisha inapaswa kufanya mabadiliko kisheria au la katika kuijengea uwezo.

Alisema kuwa katika ziara hiyo, wamepata fursa ya kukutana na Mwenyekiti wa Bodi ya TBS na wanashukuru kwa ushirikiano waliowapa na jinsi mashirika hayo yanavyoendelea kushirikiana.

# Wanafunzi wapatiwa elimu kupinga ukatili

**Na Beatrice Shayo**

KATIKA kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani, Sauti ya Matumaini Foundation (SAMAF) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi wametoa elimu ya masuala ya ukatili wa kijinsia katika Shule ya Sekondari ya Jamhuri jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na wanafunzi hao zaidi ya 600, Mkuu wa dawati la jinsia Mkoa wa Kipolisi Ilala, Inspekta Dk. Christina Onyango, aliwataka kujiamini, kuripoti vitendo hivyo wanapofanyiwa na kujiepusha na masuala ya mitandao ya kijamii.

"Acheni kujihusisha na vitendo vya ngono katika umri mdogo kwani vitendo hivyo husababisha kupata maradhi...pia acheni kuangalia picha za ngono katika simu za wazazi wenu zinawaletea mihemko na kuwasababishia kufanya vitendo visivyofaa katika jamii," alisema na kuongeza:

"Jiepusheni na tamaa, ridhikeni na kile ambacho wazazi wanawapatia ili msije kujiingiza katika matendo mabaya ikiwamo kujiuza urithi wa kudumu na wenye faida ni elimu. Mnapofanyiwa ukatili usikimbilie nyumbani wahi hospitali au polisi, hii itatusaidia kupata ushahidi wa awali pamoja na dawa za kuzuia maambukizi au mimba," alisema Inspekta Onyango ambaye pia ni Mratibu wa Kituo cha One Stop Center Amana.

Aidha, alisema katika kituo hicho cha One Stop Center wanapokea kesi zisizopungua 20 kwa wiki nyingi zikiwa za ulawiti na ubakaji.

"Changamoto kesi zinazokuja zinazohusisha masuala ya kifamilia hua zinakwama njiani kwa sababu wanaenda kuzimalizia nyumbani jambo ambalo sio sahihi na ndio maana vitendo hivi vinaendelea kuwepo. Kwahiyo nitoe wito kwa jamii wasifumbie macho vitendo hivi, waviripoti na wasikubali kumalizana nyumbani kwani tutakaposhirikiana na wakafikishwa mahakamani itasaidia kupunguza vitendo hivi," alisema Inspekta Onyango.

Mtendaji Mkuu wa SAMAF, Penina Malundo alisema Taasisi hiyo ilianzishwa mwaka 2021 na kuanza rasmi kutoa huduma za kijamii, Juni 2022,lengo ikiwa kurudisha tabasamu kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu, walemavu kwa kuwapatia misaada mbalimbali na pia kutoa elimu ya masuala ya kujitambua kwa vijana, Ukatili wa kijinsia na masuala ya afya ya uzazi.

"Leo tumekusanyika hapa kuadhimisha siku ya wanawake duniani ambayo hufanyika Machi 8 kila mwaka katika kuadhimisha siku hii SAMAF imeamua kuja kuadhimisha na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Jamhuri kwa kutoa elimu ya masuala mbalimbali ikiwemo masuala ya ukatili wa kijinsia na hedhi salama kwa watoto wa kike.

Alisema vitendo vya ukatili wa kijinsia vimekuwa tishio nchini na kufifisha ndoto za vijana wengi hususani wanaokuwa shuleni na kuwafanya kukatisha masomo yao.

"Wengi wao wanakatisha masomo kutokana na aibu wanayoipata baada ya kufanyiwa vitendo hivyo, wengine kupata majeraha mbalimbali ya kimwili na kifikra ambayo wanaona hawana nafasi tena ya kurudi shuleni. Sasa ni wakati wa Jamii kusimama pamoja kuhakikisha tunazidi kupaza sauti zetu," alisema.

Naye, Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Jamhuri, Boniphace Mwalengo, aliwashukuru SAMAF na jeshi la polisi kwa kutoa elimu hiyo ambapo itasaidia kuleta mabadiliko kwa wanafunzi hao.

Mmoja wa wanafunzi hao, Athumani Ngoda, alisema mafunzo hayo yamewapa uelewa kwani vitu vingine hawakuvifahamu.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

# TAARIFA KWA UMMA

## KUHUISHA TAARIFA ZA NAMBA YA UTAMBULISHO WA MLIPAKODI (TIN) NA NAMBA YA UTAMBULISHO WA TAIFA (NIN)

***Dar es salaam, 10 Machi, 2023***

Kwa mujibu wa mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2022, Kifungu cha 22 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi (Sura 438) kinampa mamlaka Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kumsajili na kumpa Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) kila Mtanzania mwenye umri wa miaka kumi na nane (18) na kuendelea ambaye amesajiliwa na kuwa na Namba ya Utambulisho wa Taifa (NIN) inayotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Sambamba na hilo, mabadiliko hayo ya Sheria yanamtaka kila mwenye TIN kuhuisha taarifa zake ili ziwiane na taarifa za NIN. Utekelezaji wa Sheria hii ulianza rasmi tarehe mosi Januari 2023.

Katika utekelezaji wa Sheria hiyo, TRA inapenda kuumbusha Umma kwamba, usajili wa TIN unafanyika kwa kutumia taarifa za NIN. Aidha, kila mwenye TIN ambaye alisajiliwa awali kwa kutumia vitambulisho tofauti na kitambulisho cha NIDA, anatakiwa kuhuisha taarifa zake za TIN ziendane na taarifa zilizopo kwenye NIN.

Ili zoezi la uhuishwaji wa taarifa hizi lifanyike kwa urahisi na wepesi, inashauriwa kwamba kila mwenye TIN ambayo bado haijahuishwa, kufika katika ofisi za TRA zilizo karibu naye akiwa na Namba ya Utambulisho wa Taifa (NIN) ili taarifa zake ziweze kuhakikiwa na kuhuishwa. Kwa wale wenye NIN lakini hawana TIN, wanaweza kufanya usajili wa TIN kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Ikumbukwe kwamba huduma zote za utoaji wa TIN ni bure na rahisi. Kwa taarifa zaidi, tembelea Ofisi za TRA zilizo Karibu nawe au tumia mawasiliano yafuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| **Tovuti** | : | **www.tra.go.tz** |
| **Namba za Simu bila malipo** | : | **0800 750 075 au 0800 780 078 au 0800 110016** |
| **WhatsApp** | : | **0744 23 33 33** |
| **Barua pepe** | : | **huduma@tra.go.tz au services@tra.go.tz** |

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa na:**

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**
**TRA MAKAO MAKUU**

217316402



# Taasisi yaja na mradi kukipaisha kilimo hai

**Na Valentine Oforo**, DODOMA

TAASISI ya Tanzania Pan African Investors Association (TAPAIA) inatarajia kutekeleza mradi mkubwa wa miaka 10 wa kilimo cha mazao muhimu ya chakula na kiuchumi kwa kutumia mbinu za kilimo hai.

Taasisi hiyo ya kizalendo itatekeleza mradi huo katika halmashauri mbalimbali nchini ambapo kiasi cha hekta 2,000,000 za mazao mbalimbali zinatarajiwa kuzalishwa katika kipindi cha miaka 10 kwa ushirikiano na wadau mbalimbali, zikiwamo halmashauri zinazolengwa, taasisi za fedha, wauzaji wa mashine za kilimo pamoja na wadau wa pembejeo na viwatilifu kutoka India.

Mwanzilishi na Mwenyekiti wa Taifa wa TAPAIA, Dk. Sebastian Kingu aliiambia Nipashe jana katika mazungumzo jijini hapa kuwa mradi huo kabambe unalenga kuchochea mapinduzi ya viwanda kwa kufungua fursa kwa vijana wengi zaidi kujitosa katika uanzishaji wa viwanda vikubwa na kampuni za kuchakata mazao mbalimbali yaliyozalishwa kwa njia ya kilimo ikolojia.

"TAPAIA ilipata usajili wake wa kisheria tarehe 8 Juni 2022 na mwaka jana tulianza kufanya kazi za utangulizi, ikiwa ni pamoja na kuwatambua na kuwasiliana na wadau mbalimbali ambao tunatarajia kushirikiana nao katika utekelezaji wa mpango huu," alisema.

Aliongeza kuwa hadi sasa, taasisi hiyo inaendelea na mazungumzo ya awali na halmashauri mbalimbali za Mkoa wa Pwani zikiwamo Rufiji, Kisarawe Kibiti na Chalinze kwa ajili ya kutekeleza mradi wa majaribio.

"Tunatarajia kuanzisha mashamba makubwa ya vitalu maaalum vya kuzalisha mazao mbalimbali kwa kupitia njia za kilimo hai ili kukuza uzalishaji na upatikanaji wa vyakula vingi vya lishe na mazao tiba kwa malengo mapana ya kuwasaidia kupunguza wimbi la kuenea kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza kote nchini," alisema.

Dk. Kingu alitaja mazao yatakayolimwa wakati wa awamu ya kwanza ya mradi huo katika wilaya za Mkoa wa Pwani kuwa ni pamoja na moringa, chili na rosella.

"Kwa kuanzia, lengo letu kubwa ni kuona tunafanikiwa kulima angalau aina 20 za mimea ya tiba asili pamoja na vyakula vingine vinavyoweza kuwa na lishe bora ili kuwasaidia Watanzania kujiepusha na wimbi kubwa la kuugua magonjwa mbalimbali yasiyoambukiza kama vile kisukari, saratani, shinikizo la damu na unene kupita kiasi, magonjwa ambayo yanaweza kudhibitiwa kirahisi kupitia matumizi ya mazao mbalimbali yaliyozalishwa kwa njia ya kilimo hai," alifafanua.

Katika kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kwa tija ili kufikia malengo, Dk. Kingu alisema walikuwa kwenye mazungumzo na baadhi ya taasisi za fedha, ikiwamo benki ya NMB ili kupata mikopo ya mitaji ya kusaidi ufanisi wa mradi huo, na akaongeza kuwa lengo ni kufanya mazungumzo na taasisi nyingi za fedha nchini.

"Mbali na hayo, hadi sasa tumewasiliana na baadhi ya wauzaji wa mashine za kilimo kutoka ndani na nje ya nchi ili kupata nafasi ya kitaalamu ya kupata mashine za kisasa zitakazosaidia kulima mashamba hayo kitaalamu," Dk. Kingu.

# RAS ataka bajeti ukaguzi wa dawa

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

KATIBU Tawala Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatuma Mganga amewaagiza wakurugenzi wa halmashauri za mkoa huo kutenga rasilimali zinazotakiwa kwa ajili ya ukaguzi wa dawa na vifaa tiba ili kuwezesha wananchi kupata bidhaa bora na salama.

Dk. Mganga aliagiza hayo jana jijini hapa alipozungumza na wakaguzi wa dawa na vifaa tiba na famasia kutoka halmashauri za wilaya za Mkoa wa Dodoma kwenye kikao cha ufunguzi wa mafunzo yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) kwa ajili ya kuwajengea uelewa.

Aliwataka wakurugenzi wa halmashauri kujiweka tayari kwa kutoa rasilimali ambazo zitakazowawezesha wakaguzi hao kutoa elimu na taarifa mbalimbali zitakazosaidia wananchi kupata bidhaa ambazo ni salama na bora kwa matumizi.

Alisema kuwa rasilimali hizo zikitolewa na wakurugenzi kwa wakaguzi hao, zitasaidia kuwaelimisha wananchi katika kujiepusha na matumizi ya dawa ambazo yanakuwa yamepitwa na wakati na kwa upande wa watumiaji watajilinda na afya zao. Aliwataka wakaguzi kujiepusha na vitendo vya rushwa pale wanapogundua kwenye ukaguzi wao kuna maduka yanayouza dawa na vifaa tiba vilivyopitwa na muda kwa kuwa wakifanya hivyo, watahatarisha maisha ya watu pale watakapovitumia.

"Hapa bado kuna changamoto kwa baadhi yenu, wakaguzi wana tabia ya kupokea 'vijirushwa', naomba msikubali kwa kweli kurubuniwa, mtahatarisha maisha ya Watanzania kwa kuwa dawa hizo zimepitwa na wakati," alionya.

Pia aliwataka wakaguzi hao wanapofanya ukaguzi, washirikiane na viongozi walioko kwenye maeneo husika kama vile ngazi ya kata, vijiji, mitaa na vitongoji ili wapate elimu itakayotolewa na kuaminiwa zaidi hata kama itafikia hatua ya kuyafunga maduka yatakayobainika kuwa na dawa na vifaa tiba vilivyoisha muda wake wa matumizi.

Meneja wa Kanda ya Kati, Sonia Mkumbwa alisema malengo ya mafunzo kwa wakaguzi hao ni kuwawezesha washiriki hao kufahamu majukumu na uelewa wa kufanya kazi zao kwa ujuzi kwa kuzingatia vitendea kazi.

Mafunzo hayo yatawawezesha wakaguzi kutekeleza kazi zitakazozingatia sheria na miongozo ambayo iliyotolewa na mamlaka.

Aliwataka wakaguzi hao kufanya ukaguzi kadri ya mongozo unavyotaka, ili wapate taarifa kutoka kwa wananchi zitakazosaidia kujiepusha na matumizi yanayoleta hasara ya kiafya.

Aliwataka watu kuchukua tahadhari dhidi ya dawa wanazotumia kwa kuwa wanaweza kujikuta wananunua yaliyopitwa na wakati, hali ambayo inayowaletea madhara ya mwili.



Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Innocent Bashungwa (mwenye koti jeusi), akizungumza jambo na Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Rajab Mabele (kushoto kwake), wakati wa ziara ya kukagua mitambo ya kutengenezea vipuli vya zana na mitambo ya kilimo, kwenye shamba la Mngeta Plantation Ltd, wilayani Kilombero, mkoani Morogoro juzi. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# JWTZ watangaza ajira kwa vijana

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

JESHI la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) limetangaza nafasi za kujinga na jeshi kwa vijana wa kitanzania wenye elimu ya kuanzia kidato cha nne hadi shahada ya uzamili ambao wamemaliza mkataba wa mafunzo ya kujitolea Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na kurudishwa nyumbani.

Kaimu Mkurugenzi wa Habari na Uhusiano wa JWTZ, Luteni Kanali Gaudentius Ilonda alibainisha hayo juzi jijini hapa alipotoa taarifa hiyo kwa waandishi wa habari.

Alisema vijana wenye nia ya kuomba nafasi hizo wanapaswa kuwa na sifa mbalimbali ikiwamo kuwa raia wa Tanzania wa kuzaliwa na wenye kitambulisho cha taifa. "Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 26 kwa wenye elimu ya kidato cha nne hadi cha kidati cha sita na umri usio zidi miaka 27 kwa wenye elimu ya juu," alisisitiza Luteni Kanali Ilonda.

Sifa nyingine alisema ni lazima kijana awe na afya nzuri na akili timamu, awe Mtanzania mwenye tabia na nidhamu nzuri, hajapatikana na hatia ya makosa ya jinai mahakamani na kufungwa.

Alisema sifa zingine ni awe na cheti halisi cha kuzaliwa, vyeti vya shule pamoja na vyeti vya taaluma.

"Awe hajatumikia Jeshi la Polisi, Magereza, Chuo cha Mafunzo au Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM), awe amehitimu mafunzo ya JKT kwa mkataba wa kujitolea wa miaka miwili na kutunukiwa cheti na asiwe ameoa au kuolewa," alisema.

Aliongeza kuwa maombi yote yanapaswa kuandikwa kwa mkono na kuwasilishwa makao makuu ya jeshi Dodoma kuanzia juzi hadi Machi 20 mwaka huu yakiwa na viambatanisho.

"Viambatanisho hivyo ni pamoja na nakala ya kitambulisho cha taifa au namba ya Nida, nakala ya cheti cha kuzaliwa, vyeti vya chuo na shule, nakala ya cheti cha kuhitimu JKT na namba ya simu ya mwombaji," alisema. Alitoa rai kwa Watanzania kuchukua tahadhari kwa matapeli ambao wataibuka baada ya tangazao hilo la nafasi za kujiuga na jeshi.

"Matapeli wana njia nyingi sana, hivyo Watanzania wawe makini sana na matapeli ambao wataanza kupigia simu watu wakidai wao wana uwezo wa kuwasaidia kupata nafasi hizo," alisema.





## Mke wa Rais ahimiza wazazi kuzingatia malezi ya watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF), Mariam Mwinyi amewataka wanawake kulipa kipaumbele suala la malezi ya watoto.

Mama Mwinyi ambaye pia ni Mke wa Rais wa Zanzibar, amesema wanawake wengi wamekumbwa na taharuki ya kukimbizana na harakati za uchumi na kujitafutia maisha huku jukumu la ulezi likipewa mgongo, hali aliyoieleza inaathiri ustawi wa watoto na makuzi yao.

Mama Mwinyi aliyasema hayo jana kwenye ufunguzi wa kongamano la Siku ya Wanawake Duniani kwenye Ukumbi wa Sheikh Idrisa Abdul Wakil, Kikwajuni, Zanzibar.

Alisema mwanamke ana wajibu mkubwa wa ulezi wa familia na jamii, hivyo katika mipango yake yote anayojipangia, lazima atenge muda kwa ajili ya watoto wake.

"Katika mipango yote tunayoipanga, lazima tuhakikishe tunazungumzia nafasi ya malezi kwa watoto tunapokimbizana na uchumi.

"Katika miaka hii ya karibuni pametokea mwanya wa malezi kwa watoto, lazima tutenge muda kwa ajili ya watoto wetu, haijaalishi nafasi gani mwanamke yupo kwenye harakati zake, uwe waziri au mkurugenzi tuhakikishe watoto tunawapa nguvu na tunawaelekeza," alisisitiza.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa katika harakati za kukabiliana na usawa wa kijinsia na kujikwamua kiuchumi kwa hali zote, kuna haja kujua wajibu wa ulezi kwa watoto.

"Tusije tukakimbizana sana hili jambo la malezi tukalisahau. Mwalimu wa kwanza duniani kwa mtoto ni mama, ni sisi ndio tunaobaki nao nyumbani, mama ndiye rafiki bora kwa mtoto," alisema.

Aliwataka wanawake kuzitumia fursa zinazopatikana kupitia teknolojia ya kisasa kwa kujitangaza kibiashara na kutumia soko la kimtandao kwa ajili ya kutangaza bidhaa na kazi za vikundi vyao ili kupata maendeleo ya haraka.Pia aliwashauri wazazi na walezi kuwashawishi watoto wapende masomo ya sayansi ili kuwajenga mapema kuwa watoto wazuri wa teknolojia ya baadaye.

Alisema wazazi na walezi wanapaswa kumtumia Rais Samia Suluhu Hassan kama mfano bora kuzifikia ndoto za watoto wa kike kwa kuwapa moyo ili wawe na bidii kwenye masomo yao na kufuata nyayo zake.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Uchumi, Ali Suleiman Mrembo alisema serikali ina dhamira njema kuhakikisha usawa wa kijinsia unakwenda sambamba na kuleta maendeleo ya Watanania wote.

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto, Ana Anatasi Paul aliwashauri wanawake kupitia vikundi vya wajasiriamali na kuimarisha kuitumia teknolojia kwa kujitangaza na kujitoa kiuchumi.

Alisema wanawake walio wengi bado wako nyuma na matumizi ya tenkolojia na kuwataka kuitumia fursa hiyo kujikwamua kiuchumi na kutangaza biashara zao na kulitumia vyema soko la teknolojia.

Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Khadija Issa alisema mafanikio ya shirika hilo yalichangiwa na ubunifu wa elimu jumuishi pamoja na njia za kisasa za usambazaji wa bima.

# Mwinyi aahidi neema wawekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema serikali yake inaendelea kuweka mazingira bora na wezeshi ya uwekezaji na biashara.

Aliyasema hayo jana wakati wa hafla ya uzinduzi wa mwongozo wa uwekezaji na mifumo ya kielektroniki ya Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) iliyofanyika mjini hapa.

Alisema kwa madhumuni ya kuifikia azma hiyo, serikali imedhamiria kuchukua hatua stahiki ili kuondoa vikwazo vyote vya kisheria na kimfumo vinavyozuia kuwapo mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji nchini.

"Kwa kuanzia, serikali imechukua hatua ya kuifanyia mabadiliko makubwa ZIPA kwa kukiimarisha zaidi kituo cha pamoja cha kutoa huduma kwa wawekezaji," alisema.

Rais alisema tayari jitihada hizo zimezaa matunda katika kipindi cha muda mfupi na takwimu zinaonyesha miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa kwa kipindi cha miaka miwili imefikia 226 yenye mtaji wa dola za Marekani bilioni 3.5.

Alisema miradi hiyo inategemewa kuzalisha ajira zaidi ya 13,500, hivyo matumaini yake ni kuwa mwongozo na mfumo huo utazidisha ufanisi wa utendaji wa ZIPA.

Alisema pamoja na mafanikio hayo, serikali inakiimarisha kituo hicho kwa kuweka mifumo ya kielektroniki, kurahisisha utoaji huduma na kupunguza malalamiko katika utoaji wa huduma kwa wawekezaji.

"Kama sote tunavyojua uwekezaji ni sekta muhimu kwa maendeleo ya nchi katika kukuza uchumi na kuzalisha fursa za ajira. Kwa kuzingatia hilo, Zanzibar imefungua milango ya uwekezaji kwa wawekezaji wote wa ndani na nje waje kuwekeza nchini ili kuunga mkono juhudi za serikali za kuleta maendeleo," alisema.

Waziri wa Nchi ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga aliyapongeza mashirika ya Umoja wa Mataifa katika uandaaji wa mwongozo huo na kanuni za kieletroniki, akisisitiza una mchango mkubwa katika kukuza uwekezaji Zanzibar.

Akizungumzia uwekezaji wa visiwa, waziri huyo alisema uwekezaji huo unaendelea na sehemu kubwa ya uwekezaji huo wanatarajia kabla ya mwaka 2025 uwe umekamilika.

Mkurugenzi wa ZIPA, Sharif Ali Sharif alisema mfumo huo wa kieletroniki wa kuwahudumia wawekezaji ni mwendeleo wa utekelezaji wa sera ya maendeleo ya Serikali ya Zanzibar na uzinduzi huo ni kielelezo tosha katika kukuza sekta ya uwekezaji.

Alisema taasisi zote zitafanya kazi kwa pamoja kupitia mfumo huo kuhakikisha huduma zote na maombi ya mwekezaji zinasimamiwa na kupatiwa ufumbuzi ndani ya kituo kimoja cha uwekezaji.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la ndege Tanzania (ATCL), Mhandisi Ladislaus Matindi akizungumza na waandishi wa habari, baada ya ufunguzi wa mkutano wa Baraza la wafanyakazi wa shirika hilo, jijini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZECO na ESR kutekeleza mradi umeme wa jua Pemba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini imetiliana saini na Kampuni ya ESR ya Ujerumani, kuanzisha mradi wa uzalishaji umeme wa jua visiwani Zanzibar.

Mkataba huo wa makubaliano ulifikiwa kati ya Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) na Kampuni ya ESR utakaowezesha Kisiwa cha Pemba kunufaika na nishati hiyo.

Hafla hiyo ilifanyika jana Maisara mjini Zanzibar na Waziri wa Shaibu Hassan Kaduara, akisema hatua hiyo itafungua Kisiwa cha Pemba katika uwekezaji.

Alisema Pemba inapata umeme kutoka Tanga wa Megawati 20 na kwamba ujio wa umeme wa jua kutasaidia kisiwa hicho kuwa na nishati mbadala.

Waziri huyo aliitaka kampuni ESR ya Ujerumani kufanya kazi hiyo kwa ubora ili kufikia lengo la kuwa na umeme wa uhakikika ambao matumizi yake hayana gharama kubwa.

Alisema wizara imejipanga kuhakikisha kuwa mradi huo unakamilika kwa wakati ili kuleta mafanikio makubwa kwa wananchi wa Zanzibar.

Alisema licha ya kuwapo kwa umeme kutoka Tanga wa Megawati 20 hautoshelezi mahitaji ya wakazi hao, hivyo ujuo wa huduma hiyo utasaidia kutosheleza uhitaji.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Josehp Kilangi alisema kukamilika kwa kituo cha usambazaji umeme wa jua kwenye Kisiwa cha Pemba kumetoa fursa kuwapo uhakika wa huduma.

Katibu Mkuu wa ESR, Siluvio Hauenchild, alisema kampuni yake imejipanga kufanikisha ujenzi wa kituo hicho ili kuleta maendeleo kwa wananchi wa Pemba na wawekezaji.

Alisema kuwa tayari wameshafanya utafiti na kubaini kuwa mradi huo kwa Kisiwa cha Pemba utakuwa bora na kuleta mafanikio kwa wananchi na unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwaka huu.



**GIGY MONEY**
UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT

JUMAMOSI MACHI 11, 2023



# KAWA 'FITI' MTAKOMA

STAA wa muziki wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, ameanza kuimarika haraka na kuwatoa hofu mashabiki wa Bongo Fleva ambao walionekana kuhoji kuhusu kuporomoka kwa afya yake.

Hivi karibuni msanii huyo kupitia ukurasa wake wa Instagram, ameweka video ambayo anaonekana akipima uzani na majibu yake yalimshangaza.

Katika matokeo ya upimaji uzani huo, Diamond alikuwa na uzito wa kilo 73.9 ambao kwake ulimshangaza.

Diamond alionyesha wazi kuwa uzito wake mpya ulimshangaza kwani hakutarajia kufikia hapo.

"Doh! 73.9kg," aliandika chini ya video ambayo inamuonyesha akiwa amesimama juu ya kifaa cha kupima uzito wa mwili.

Novemba mwaka jana, baadhi ya mashabiki walionyesha wasiwasi kutokana na muonekano wa msanii huyo, na yeye mwenyewe aliweka bayana kwamba haelewi nini kinachosababisha mwili wake kupungua.

Akitumia mtandao wa Instagram, alionekana naye akishangaa kwa mwili wake kuendelea kupungua kadiri siku zinavyokwenda.

"Halafu nimekuwa mdogo kila siku nazidi kuwa mdogomdogo. Hilo suala linawachanganya Watanzania wengi," aliandika Diamond Platnumz.

BASI SAWA

## DJ Joozey hunaga maringo



MCHEZESHAJI muziki maarufu, DJ Joozey ameeleza kutengeneza kwake kipande cha video kwa ajili ya Harmonize, inatokana na upendo wa dhati kwake.

Video hiyo aliitengeneza baada ya kufanikiwa kupanda Mlima Kilimanjaro na kupiga muziki kileleni kwa muda wa dakika 15.

DJ Joozey amesema kuwa amefanya hivyo kwa upendo alionao kwa Harmonize kwa kuwa amemsaidia sana kwenye maisha yake.

## Mayenje kuja na filamu mpya

MSANII nguli wa filamu nchini Novatus Mayenje amesema anatarajia kuachia filamu mpya ambayo itashirikisha wasanii chipukizi na wakongwe.




Akizungumza na kona ya burudani alisema filamu hiyo itakuja na sura mpya kutokana na vionjo vilivyopo.

"Muda wowote kuanzia leo ninatarajia kuachia filamu yangu mpya wadau wasubiri kuona vitu vipya huwa sifanyi kitu kwa kubahatisha,alisema Mayenje.

Alisema atatoa jina la filamu mara tu itakapokamilika pamoja na kuomba mashabiki wake waipokee kwa mikono miwili.

Alitaja baadhi ya wasanii aliowashirikisha kuwa ni Chuchu Hans, Mtanga, Tea na Ray Kigosi.



## GIGY WEWE NI NOMA!

MWANAMUZIKI mwenye utata, Gigy Money, amesema katika maisha yake akimtamani mwanaume anamkabili na kumtongoza.

Amesema kutokana na kujiamini hawezi kuishi kwa kumtegemea mwanaume kwa sababu anamuona ni kiumbe cha kawaida na anayeweza kuambiwa chochote.

Gigy Money amesema kuna baadhi ya watu wanaodai kwamba yeye ni mdangaji ili aendeshe maisha yake, jambo ambalo si la kweli kwani yeye anajimudu kimaisha na ndio maana hatishwi na wanaume.



## Makabila amkataa kiaina Anjella

MSANII wa muziki wa Singeli, Dulla Makabila amekanusha kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Annjella akisema wao ni kama marafiki wa kawaida.

Hata hivyo, Makabila ameshangaa kusikia kwamba yeye na Anjella walionekana Zanzibar wakila bata.

"Sijakwenda Zanzibar na Anjella, hizi habari sijui zinatoka wapi, mimi na yeye ni marafiki wa kawaida na tunapokutana tujadili vitu vya kawaida na sio mapenzi," amesema Makabila.

## WASANII WANAOTUMIA MAJINA 'ORIGINAL'

**Na Adam Fungamwango**

KARIBU asilimia 70 mpaka 80 ya wasanii wengi wa muziki duniani hujulikana kwa majina yao maarufu ya kisanii na wala si yale halisi.

Wasanii wengi duniani hutumia majina ya kutungwa na mashabiki au kujitungia wenyewe, yakiwa ama yanalingana na kile kitu wanachokifanya, au kifupi cha majina yao.

Lengo ni kufanya majina yao kutamkika vizuri, tofauti na baadhi ya majina halisi ambayo mengine ni marefu na hayaonekani kuwa na mvuto mbele ya wanaoyasikia.

Hawa ni baadhi ya wasanii wa Kitanzania wa bongo fleva maarufu nchini ambao wanatumia majina yao halisi, lakini bado wamekuwa na ushawishi kwa mashabiki kila kona.

**Ali Kiba**

Ni msanii staa zaidi nchini Tanzania ambaye anatumia jina lake halisi. Ni nembo ya muziki wa bongo fleva Tanzania aliyeingia kwenye fani hii mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Kiba ameingia kwenye muziki wa bongo fleva kwa bahati tu, kwani ni mchezaji soka mzuri sana na ilikuwa asajiliwe na moja kati ya timu za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hata hivyo pia alikuwa anajishughulisha na muziki wa kizazi kipya na tayari alikuwa amesharekodi ngoma ya 'Cinderella'.

Ilipohiti alikwenda kupiga shoo Mwanza, baadaye akazunguka nchini nzima, hapo ndoto za kuwa mwanasoka maarufu nchini zikafa.

**Vanessa Mdee**



Pamoja na kwamba jina lake la pili ni la kikabila, lakini hakujali hilo. Anajitambulisha kwa majina yake yote mawili. Na hata mashabiki wake wanamfahamu kwa majina yake yote. Ukimuuliza mtu msanii 'Vanessa'. Atakuuliza tena Vanessa Mdee?

Utafiti mdogo umefanywa na kugundulika kuwa wasanii wengi wa kike ndiyo wanaoongoza kwa majina ya kubuni. Lakini siyo kwa huyu.

**Aslay Isihaka**

Jina lake halisi ni Aslay Isihaka Nassor. Mwanzoni alijiita Dogo Aslay. Jina ambalo pia halikupindisha jina lake halisi. Na hata sasa ameendelea kujitambulisha kwa jina lake.

Mmoja ya wasanii vijana kabisa ambao wamekuwa mastaa akiwa wa umri mdogo.

**Nandy Mfinanga**

Anaitwa Nandy. Yeye hujitaja kwa jina moja tu, tofauti na Vanessa Mdee. Ndiyo maana hakuna hata mmoja anayejua kama anaitwa Nandy Mfinanga. Ni mmoja ya wasanii wa kike vijana ambao wamekuwa mastaa nchini wakiwa na umri mdogo.

**Mrisho Mpoto**

Ni mwimbaji, mtunzi na mshairi. Ana aina yake ya staili ya uimbaji wake ambao ni wa kughani mashairi. Amejipatia umaarufu mkubwa kutokana na aina yake hii ya muziki ambao maneno na ujumbe wake unafikirisha zaidi kuliko kukupa burudani ya kucheza.

Kutokana na aina yake ya muziki, muonekano, mavazi yake, na hata staili yake ya maisha, wala isingekuwa rahisi kwake kutumia jina la kubuni na kuachana na jina lake halisi.

FILAMU

## Siri ya ndoa: Haina siku ya kuzaliwa

**Na Adam Fungamwango**

NDOA siyo sikukuu ya kuzaliwa, wazungu wanaita 'birthday'. Sikukuu ya kuzaliwa unaweza kuifanya kila mwaka, lakini si ndoa. Hufanyika mara moja tu, au ni kitu nadra sana kutokea kwenye maisha ya mwanadamu. Ndiyo maana inashauriwa kuwa yeyote anayetaka kuingia kwenye taasisi hiyo awe amejipanga, kiuwezo wa kimwili na kiakili. Ndoa ni kujikana mwenyewe, kujipunguzia kujipenda zaidi wewe. Unatakiwa kuijali zaidi familia kuliko wewe mwenyewe. Kujipunguzia mamlaka ya kwenda sehemu yoyote na muda wowote unaoutaka bila sababu za msingi.

Wapo wanaooa au kuolewa kwa sababu ya kuona wenzao wamefanya hivyo na amebaki yeye, hivyo anataka kufanya kwa ajili ya kufuatisha wenzake. Hiyo ndoa haitodumu kamwe.

Tukiangalie filamu ya 'Siri ya Ndoa', iliyochezwa na Dora Martin, Zena  Mkima, Hawa Ramadhani, Nassor Chilumba, Rayuu Chande, Verena Mathayo.

Rajab anataka kuoa. Anamfuata dada yake Havintishi na kumweleza azma yake hiyo. Dada yake anakuwa na wasiwasi na hilo.

Anamuuliza kama ataacha tabia yake ya kupigapiga watu, maneno mengi na gubu. Kwa sababu anahitaji, Rajab akaahidi kuishi vema na huyo mwanamke. Anamuoa Rabiya. Hata hivyo inakuwa ni ndoa ya misukosuko. Mwaka unapita Rabiya hajashika ujauzito.

Badala ya kubembelezana, Rabiya anapokea kichapo, matusi, dharau na kejeli kutoka kwa mumewe. Kama vile haitoshi msichana wa jirani Leila anaiingilia ndoa yao. Rajab sasa anakuwa haoni hasikii kwa Leila.

Licha ya kutoshika ujauzito, dada wa Rajab Havintishi anakuwa upande wa wifi yake. Anapambana na kaka yake kila kukicha juu ya kumnyanyasa mkewe. Mwisho wa siku anaamua kumchukua na kukaa naye nyumbani kwake kumuepusha na vipigo.

Havintishi anaendelea kupambana na ndoa ya kaka yake, anamfuata Leila na kumchimba mkwara wa hali ya juu, akimwambia aachane na kaka yake, la sivyo atamuonyesha.

'Biti' alilopigwa linamuogopesha Leila anaamua kuvunja uhusiano wake na Rajab. Haamini macho yake, anaamua kwenda kwao ukweni kumfuata mkewe Rabiya hamkuti. Wanamjibu hajawahi kufika huko, labda yupo kwa mwanaume mwingine. Rajab anachanganyikiwa. Ukweli ni kwamba wanajua alipo. Yupo kwa Havintishi dada yake Rajab. Baadaye anapelekwa huko. Alipofika alimuomba radhi dada yake Havintishi na mkewe Rabiya na kuahidi kubadilika. Rabiya anamsamehe mumewe.





# Omotola huwezi kumsahau baba

MKONGWE wa uigizaji nchini Nigeria, Omotola Jalade-Ekeinde, amezungumzia madhara yaliyosababishwa na kifo cha baba yake mzazi.

Katika mahojiano maalum na Chude Jideonwo, mwigizaji huyo aliyejizolea umaarufu, baba yake alifariki akiwa na umri wa miaka 12, lakini siku hiyo alipatwa na hofu baada ya kuona watu wanakusanyika nyumbani kwao.

“Nilianza kuona umati wa watu nilipofika mtaani kwangu na nilijua, hakika kumekuwa na kifo. ilikuwa kama sinema. Ilinibidi nitembee katikati yao. Kila mtu anageuka kukutazama, wengine wakilia. Wengine wakitazama kwa mwendo wa polepole, bado nakumbuka hisia zile,” amesema.



## Oji amemaliza mwendo

MWIGIZAJI mkongwe wa Yoruba, Ojo Arowosafe, maarufu kama ‘Fadeyi Oloro’, amefariki dunia.

Kulingana na taarifa zilizopatikana jana, mwigizaji huyo alikufa Jumanne jioni baada ya kusumbuliwa na maradhi ya muda mrefu.

Fadeyi alikuwa mmoja ya wasanii wazuri kwenye skrini katika tasnia ya sinema za Kiyoruba, anayejulikana kwa uso wake wenye hasira na utumiaji wa bunduki kwa ajili ya kusuluhisha mizozo.

## Hakuna siri tena

HAKUNA siri tena kuhusu uhusiano wa kimapenzi kati ya Kendall Jenner na Bad Bunny, baada ya picha inayowaonyesha wakiwa pamoja kimahaba kusambaa mitandaoni.

Mwanamitindo huyo na mwimbaji nyota wa Reggaeton walikuwa wakila bata na rafiki zake pamoja na Kylie Jenner hivi karibuni .

Wawili hao wameonekana wakitembea huku wamekumbatiana katika eneo la watu mashuhuri jijini NewYork.





## Regina ukweli una machungu

MSANII wa filamu kutoka Nollywood, Regina Daniels amewataka watu mashuhuri na watayarishaji wa filamu kukomesha vitendo vya kuwatumikisha watoto katika tasnia ya burudani.

Katika video ya hivi majuzi aliyoshirikisha kwenye ukurasa wake wa Instagram, mwigizaji huyo alisema unyanyasaji wa wasichana wadogo unavyoweza kuathiri vibaya ustawi wao wa kiakili na kimwili. Daniel alibainisha kuwa anaelewa jinsi tasnia hiyo ilivyo hatari kwa wanawake, hata yeye aliokolewa kwa sababu ya ushawishi wa mama yake.

## Simi yuko nao wanaosaka maisha

MWIMBAJI na mtunzi wa nyimbo kutoka Nigeria Simi, ametoa maoni yake kuhusu kwa nini Wanigeria wengi wana tabia ya kuhama hama kutafuta pesa.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter amesema hakuna mtu anayetaka kuwaacha marafiki na familia zao nyuma, lakini hawataki kufa wakiwa mafukara.

“Waafrika weusi inabidi wapigane na kupigania nafasi na heshima na kuishi kila mahali wanakoenda kwa sababu sehemu moja ambayo ni haki yao ya kuzaliwa ni ngumu kuendesha maisha yao,” ameeleza.





## Mradi kunufaisha wakulima 8,000

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAKULIMA 8,000 wa mbaazi mkoani Manyara wataanza kunufaika na tija ya mradi wa kuhamasisha uzalishaji na ulaji bora wa mbaazi ili kuliongezea thamani zao hilo na kumsaidia mkulima kufurahia matokeo ya jasho lake.

Mpango wa kuwainua katika uzalishaji wakulima hao ulibainishwa jana na Mshauri wa Mambo ya Kilimo na Biashara, Neema Nassary kutoka Shirika la RIKOLTO, alipouzungumzia mradi huo.

Alisema mradi huo unaohamasisha matumizi bora ya chakula kinachotokana na mbaazi, unatekelezwa kwenye Halmashauri ya Mji wa Babati na Halmashauri ya Wilaya ya Babati, mkoani Manyara.

"Kiujumla, mradi huu umeanza tayari tangu mwezi Desemba mwaka jana, na utafikia ukomo wake Juni mwaka huu. Mikoa mingine inayotekeleza mradi huu ni Arusha, Manyara, Morogoro, Dodoma na Dar es Salaam.

"Tunautekeleza mradi huu pamoja na watoa huduma za hoteli na kwenye mikutano, mamalishe, babalishe, shule, magereza na hospitali.

"Kimsingi, tumepanga kutumia AMCOS (Vyama vya Msingi vya Wakulima wa Mazao) ili tuwape elimu wakulima juu ya ulaji wa mbaazi ambayo itainua uchumi wao," alisema Neema.

Kwa mujibu wa mshauri huyo wa RICOLTO, mbaazi za Babati na Karatu ni nzuri, kwa kuwa hazichagui hali ya hewa, ndio maana walichagua kutekeleza mradi huo kwenye maeneo hayo.

Alipoulizwa kuhusu soko, alisema mapishi wanayowafundisha wakulima, ndio yatakuwa mwarobaini wa kusaidia kuongeza soko la mbaazi.

"Kuna mapishi aina 20 ya mbaazi ikiwamo uji wa mbaazi, biriani ya mbaazi, maandazi, hafu keki, donati, supu ya mbaazi, futari ya mbaazi na mbaazi za ndizi," alibainisha.

# Filamu Royal Tour yaongeza watalii, mapato ya Saadani

**Na Cynthia Mwilolezi,** TANGA

UONGOZI wa Hifadhi ya Taifa Saadani umepongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa ubunifu wa kutengeneza filamu ya Tanzania The Royal Tour, ukibainisha kuwa imechochea ongezeko la wageni na mapato yao.

Akizungumza jana na Nipashe kwenye hifadhi hiyo, Kaimu Mkuu wa Hifadhi hiyo, Gabriel Genda alisema wanayo fahari ya kujivunia kuwa na Rais Samia ambaye ameipaisha hifadhi hiyo kwa ubunifu wake.

Alibainisha kuwa kwa mwaka 2019/20, walipata wageni 13,865 waliotembelea hifadhi hiyo; wa nje ya nchi walikuwa 2,983, wazawa 10,489 na wageni wakazi 393.

"Watalii hawa waliingizia serikali zaidi ya Sh. milioni 682. Tukiutazama mwaka wa fedha 2020/21, tulipokea wageni 20,840.

Kati yao, wa nje 3,430, wazawa 16,839 na wageni wakazi 571 na kupata zaidi ya Sh. milioni 734," alisema.

Alibainisha kuwa kwa mwaka 2021/22, walipokea wageni 28,355. Kati yao, wa nje walikuwa 4,308, wazawa 23,451, wageni wakazi 596 na kuingiza zaidi ya Sh. bilioni moja.

"Wageni hawa tunaona wazi idadi inaongezeka, hasa wazawa baada ya jitihada za Rais Samia kutangaza vivutio vyetu nchini kupitia filamu ya Tanzania The Royal Tour. Tunaamini idadi itaongezeka zaidi," alisema.

Alilishukuru Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kwa jitihada za kuboresha miundombinu ya hifadhi kuhakikisha wageni wanaotembelea vivutio wanapata huduma bora na salama.

Genda alitaja vivutio wanavyotembelea Hifadhi ya Taifa Saadan ni utalii wa boti ambao huwezesha kuona makundi makubwa ya familia za viboko na mamba ndani ya Mto Wami.

Vivutio vingine ni kuona wanyama usiku, utalii wa kutembea kwa miguu hifadhini, utalii wa fukwe zenye kasa wa kijani na mchanga wa Fungani.



Ofisa Mtendaji mwanamke wa kata ya Ngomeni, wilayani Muheza, mkoani Tanga, Kabula Joseph akiijaribu moja kati ya pikipiki tisa mpya zilizotolewa na serikali kwa maofisa watendaji wa wilaya hiyo juzi, kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi. Kushoto ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Erasto Mhina na (kulia) ni Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Emigidius Kasunzu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wajumbe Baraza Wawakilishi waridhishwa miradi ya TASAF

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WAJUMBE wa Kamati ya Kuisimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, wameridhishwa na utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwenye Halmashauri ya Meru mkoani Arusha.

Wajumbe hao wameridhishwa na ujenzi wa miradi ya TASAF, inayotekelezwa kwa ufadhili wa Umoja wa Nchi Zinazozalisha Mafuta Duniani (OPEC).

Akizungumza jana wakati wa mkutano wa hadhara na wananchi wa Kandashe na wanufaika wa mradi huo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Machano Othman Said, alisema wajumbe wa kamati hiyo wamekwenda kuangalia miradi ya afya na elimu ili kujifunza namna ujenzi ulivyofanyika.

"Wananchi wa Arumeru mmebahatika kupata miradi hii mikubwa na mizuri hasa ya OPEC ukizingatia Tanzania ni nchi kubwa na kuna mahitaji mengi," alisema.

Alibainisha kuwa kwa Zanzibar, miradi ya TASAF, hasa ya ujenzi wa miundombinu, imetekelezwa vizuri, hivyo serikali imefanya vizuri wananchi wanapaswa kuipongeza na kuiunga mkono. "Ndugu wananchi, ninawaomba tuhakikishe tunalinda miradi hii na inapotokea kasoro ndogo, mfanye ukarabati ili idumu kwa muda mrefu kwa maslahi ya kizazi cha sasa na cha baadaye," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo na Mwakilishi wa Bumbwini, Mtumwa Pea Yusuph, alisema amefarijika kuona namna miradi hiyo ilivyotekelezwa kwa viwango na usimamizi bora na makini.

"Serikali imefanya kazi nzuri tunapaswa kuiunga mkono kwa kuwa viongozi wetu wamefanya kitu ambacho kimegusa maisha ya watu moja kwa moja ikiwamo kuwakwamua kiuchumi," alisema.

Katika ziara hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Emmanuela Kaganda alisema serikali kupitia TASAF, imetoa fedha za ujenzi wa miradi ili kuhakikisha wanaimarisha maisha ya wananchi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kandashe, Arodi Mafie alisema awali wananchi walikuwa wakiteseka kupata huduma za afya kwa kuwa walitembea umbali mrefu hadi Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro kwenda kutafuta matibabu.

Abel Palangyo alisema alianza kunufaika na mradi huo tangu mwaka 2015 na umemsaidia kusomesha watoto na kupata kwa urahisi huduma za uhakika za matibabu baada ya kujengewa Zahanati.

Marry Kitomari alisema kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini, amenufaika kwa kuboresha kipato cha familia kwa kuwa fedha alizopokea alizitumia kununua mbuzi na kuku ambao wamemsaidia kujikwamua kiuchumi.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Maisha zama zile, mzazi anawafunza watoto wote kuanzia kupika, kila kitu nyumbani

**Na Adam Fungamwango**



WE mtoto we kaza mkono huo, kaugali kenyewe 'ka peke yako unakapika utafikiri nini, utakuja kuwa mkubwa, uwapikie watoto wako, mumeo na mkweo. Kama hivyo shoga 'angu si utawapikia wakwezo ugali mbichi."

Nakumbuka, haya ni baadhi ya maneno ya kinamama wa zamani wakati wa kuwafundisha mabinti zao kusonga ugali, na si ugali tu, lakini hata vyakula vingine.

Hata hivyo mara nyingi kinamama wa zamani walianza kuwafundisha watoto stadi za kazi wakiwa bado wadogo. Waliwafundisha kufua nguo zao wenyewe taratibu. Anaanza na kumpa moja tu afue. Waliwafundisha kupika na hasa walianzia ugali. Halafu mboga ambazo upishi wake ni rahisi kama mlenda, dagaa na kadhalika.

Zamani iwe mjini au vijijini mtoto wa kike anapotoka shuleni ni mara chache sana kukuta amefunikiwa chakula. Itakuwa hivyo kwa sababu za msingi sana. Na wala siyo kwa sababu ametoka shule. Wazazi wa zamani hawakumuwekea chakula mtoto eti kwa sababu ametoka shule tu. Tayari kuna kazi zingine za nyumbani unatakiwa kufanya ili upate chakula, au ulishazifanya kabla ya kwenda.

Watoto wa kike wanaporudi shuleni, wanaweza kukuta mboga ipo jikoni. Hapo mama sasa ataacha kazi hiyo na kuendelea na shughuli zake zingine. Mapishi anaachiwa msichana. Atamalizia mboga na baadaye atapika ugali. Uwe wa kwake peke yake, au wa familia nzima.

Huyu mtoto anayeweza kupika ugali leo anakuwa ameandaliwa muda mrefu. Mama anapokuwa anapika anawaita watoto wa kike na kuwaambia "angalieni ninavyopika hapa."

Watoto watamuangalia, halafu baadaye wataanza kujifunza na wao. Na mara nyingi hujifunza kupika ugali wao wenyewe wanapotoka shuleni.

"Pika ule hata uwe mbichi si wa kwako mwenyewe." Mama atamwambia binti yake. Anaweza kupika mbichi leo, akala, lakini baada ya wiki moja tu, hali inabadilika.

Baadaye taratibu mabinti wanaanza kupika ugali hata wa watu wawili na hatimaye familia nzima, wengine wakiwa na umri mdogo tu wa miaka saba hadi 10.

Miaka 10 hadi 15 watoto wa kike wa zamani waliweza hata kuachwa na mama zao nyumbani, wakaenda shamba, au kusafiri hata wiki nzima, akarudi akaikuta nyumba ipo salama kabisa.

Msichana anampikia baba yake, kaka zake na ndugu wote, anaosha vyombo, anachota maji, anasafisha nyumba na kufua.

Hapa mzazi wa kike anajisifia moyoni kuwa kweli sasa nimezaa na nimekuza, na sasa anamuona binti yake huko mbele ya safari anaweza kuitunza familia yake atakayoianzisha.

Wengine hufundishwa na bibi zao, shangazi na ndugu wengine.

Watoto wa kiume hao halikadhalika. Kinababa wa zamani siku za mapumziko walikuwa na tabia ya kuvaa fulana nyepesi zenye mikono iliyokatwa na kamptura aina ya bichimoma, au msuli. Atakaa kwenye kiti chake varandani, au chini ya mti anasoma magazeti yake, lakini baada ya hapo anaweza kuchukua kwanja lake, atazunguka nyuma na kuanza kukata majani ambayo yameanza kuchomoza kuzunguka nyumba yake.

Baada ya hapo ataita mtoto au watoto zake wa kiume wayazoe na kwenda kuyatupa sehemu maalum iliyotengwa.

Wakati mwingine mzee anaweza kuchukua watoto wake, akazunguka nao nyuma na jembe mkononi na kuwaelekeza wachimbe sehemu fulani.

Inawezekana sehemu hiyo ni mtaro ambao anataka maji yawe yanapita.

Watachimba mpaka hatua fulani, halafu atawaambia wapumzike na yeye anamalizia.

Haya ndiyo maisha ya wazazi wengi wa zamani. Waliwafundisha watoto wao kazi mbalimbali wakiwa bado wadogo sana. Wakati mwingine watoto wanaweza kuona kama ni mchezo tu wanacheza au mazoezi kwa sababu bado wadogo. Au kuna wengine wakaona kama wanateswa tu hivi na hasa wale wanaofanyishwa hivyo na walezi ambao hawakuwazaa.

Lakini ilikuwa inawajenga sana kwa sababu baadaye wanakuja kukutana na mambo kama hayo kwenye maisha yao halisi.

Kumekuwa na malalamiko mengi kwa sasa kuwa vijana wengi wa kizazi hiki ni wavivu na hawapendi kazi, hasa zile ngumu. Wanapenda kazi nyepesi, ikiwemo za kukaa tu ofisini, dukani au zinazofanana na hizo ambazo wala hawana elimu nazo, au uwezo.

Ni kwa sababu hawajazoweshwa kazi za mikono tangu wakiwa wadogo. Zile kazi zilifanya watoto wengi kuwa wabunifu na uwezo wa kujitegemea wakati mwingine wakiwa bado wadogo tu wa miaka 18. Ndiyo maana vijana wengi wa zamani ambao kwa sasa ni watu wazima walikuwa na uwezo wa kuondoka kwao kwenda mikoa ya mbali kujitegemea, tena kwa kufanya kazi ngumu bila kuchagua.Pamoja na kwamba vijana wengi wa sasa wengi wamesoma na wana elimu kubwa kuliko wa zamani, lakini wanakosa elimu ya stadi za kazi.

Hata waajiri siku hizi wamekuwa wakilalamika kuwa wahitimu, pamoja na vyeti vyao vizuri, lakini uchapaji kazi wao umekuwa hafifu.

Kwenye miaka ya karibuni ndiyo tumeanza kushangaa kusikia eti msichana mkubwa tu, hawezi kupika hata ugali. Ilikuwa ni ajabu miaka hiyo kusikia hivyo.

Kuna picha moja 'iliyotrendi wiki hii kwenye mitandao ya kijamii msichana mdogo wa miaka ipatayo saba hivi akisonga ugali kwenye mafiga. Unaonekana kabisa ni wa familia, na alikuwa akiusonga kwa swaga, kwanza ilionekana pamoja na udogo wake ni mzoefu, lakini anapenda anachokifanya.

Ujumbe mfupi wa watu ndiyo ulinishangaza sana. Kinadada wengi walikiri kuwa hawawezi kusonga ugali kama alivyokuwa akifanya mtoto yule. Wengine wakasema siyo wao tu hata watoto wao hawawezi. Wakaonekana kushangaa na kumpongeza. Ndipo nilipojua kuwa tuna kizazi cha aina gani. Kumbe watoto wa aina ile wamebaki wachache sana. Yale ni malezi tu.

Kuna sehemu baadhi ya wazazi walikengeuka. Wakaanza kuwadekeza watoto wao wakidhani wanawapenda. Wakajaza mahausigeli na hausiboi huku wakiwaacha watoto wao kutosuuza hata kikombe alichonywea chai au sahani aliyolia chakula.

Matokeo yake tunapata kizazi cha aina hii. Hakitaki kazi ngumu, lakini kinataka pesa nyingi. Hakijui kupika wala kufua.

Unaweza ukawa umesoma sana na una elimu kubwa, lakini kama mtu hawezi kufanya kazi yoyote ya mikono, utakuwa na matatizo makubwa kwenye maisha yako hata kama una pesa kiasi gani.

**Tuma meseji 0716 350534**

# Wadau wasema dhamira yake inaonekana kwenye matendo

Na Restuta James

WAKATI Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akitimiza miaka miwili madarakani mwezi huu, kasi ya uwekezaji katika sekta ya nishati imemwibua waziri wa zamani wa Nishati na Madini, William Ngeleja, aliyesema ‘dhamira yake tunaiona kwenye matendo zaidi.’

Akizungumza na Nipashe jana, Ngeleja ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Sengerema (CCM), alisema uzalishaji na usambazaji wa nishati ya umeme umedhihirisha namna ambavyo Rais Samia yuko tayari kuhakikisha Tanzania inapiga hatua ya maendeleo.



“Tumeona commitment (utayari) za kifedha ambazo yeye kama kiongozi mkuu wa nchi anasaidia Wizara ya Nishati, Wakala wa Umeme Vijijini (REA) na Shirika la Umeme (TANESCO), inatia moyo dhamira yake tunaiona kwenye matendo zaidi na tunampongeza sana,” alisema.

“Ni rai yangu kwa kila Mtanzania tumwombee mema ili aendelee kutekeleza haya ambayo ameyakusudia.”

Alisema kufunguka kwa sekta nyingine kunachangiwa kwa kiasi kikubwa na upatikanaji wa uhakika wa nishati ya umeme mijini na vijijini.

Akizungumzia ujenzi wa Bwawa la Nyerere (JNHPP), lililoko mto Rufiji, mkoani Pwani na ahadi ya Rais Samia ya kufikisha umeme vijiji vyote ifikapo Desemba mwaka huu, Ngeleja alisema ni mambo ambayo yatafungua nchi kwa kiasi kikubwa.

“Nchi inatembea, tunapiga hatua kubwa ya kimaendeleo kwa sababu wote tunafahamu nishati ya umeme ni nyenzo muhimu sana katika maendeleo yoyote,” alisema Ngeleja.

Wachambuzi wa masuala ya maendeleo wanaeleza hatua ya kuzalisha umeme na kuusambaza kwa wananchi itatengeneza ajira nyingi za moja kwa moja na zisizo rasmi hususani vijijini.

Wachambuzi hao waliiambia Nipashe kumekuwa na kampeni ya matumizi ya nishati rafiki kwa mazingira jambo ambalo litaibua ubunifu kwenye sekta hiyo.

Kamishna wa zamani wa madini, Dk. Peter Kafumu, alisema uwekezaji unaofanywa na serikali unachochea maendeleo ya haraka mijini na vijijini.

Akizungumza na Nipashe jana, Dk. Kafumu, alisema azma ya serikali kufikisha umeme katika vijiji vyote ifikapo Desemba mwaka huu, itazalisha ajira nyingi na kupunguza idadi ya vijana wanaohamia mijini.

Alisema kazi ya kuimarisha gridi ya taifa itawasaidia wananchi wa vijijini kuwa na uhakika wa umeme na hivyo shughuli za biashara zitafanyika kwa urahisi.

Dk. Kafumu ambaye amewahi kuwa mbunge wa Igunga (CCM), alitoa mfano wa mwaka 2012 serikali ilipeleka umeme katika moja ya vijiji vyenye bwawa la samaki kijijini kwake, ambao uliibua fursa nyingi za biashara.

“Vijana walikuwa wanachomelea vitu mbalimbali, wanawake walianzisha biashara ya mabarafu ambayo waliwauzia wavuvi kwa ajili ya kuhifadhi samaki...unaweza kuona kwamba ni watu wangapi walikuza kipato,” alisema.

> **“Miradi hii ina maana kubwa sana kwa wananchi hasa vijijini na taifa kwa jumla, ndiyo maana inapelekwa katika maeneo ya madini, kilimo, viwanda vidogovidogo na vituo vya afya. Ukitaka kuwasaidia wanyonge, wafanyie mambo yao yawe mazuri na ndicho tunachokifanya,” alisema Rais Dk. Samia.**

Alipongeza kazi inayofanywa na Rais Samia akisema umeme unachagiza maendeleo ya sekta nyingine nyingi.

Kuhusu siasa, alisema Rais Samia amefanya vizuri zaidi kwenye eneo hilo akisema ‘nchi imepoa’ na kwamba kitendo chake cha kuhudhuria sherehe za Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA) kinaongeza wigo wa kutoa maoni kwa wananchi.

Mwishoni mwa mwezi uliopita, Dk. Samia alisema vijiji vyote nchini vitakuwa vimepata huduma za umeme ifikapo Desemba, mwaka huu.

Aliyesema hayo alipokuwa akishuhudia utiaji saini wa mikataba 26 ya utekezaji wa miradi ya umeme katika maeneo ya miji na vijiji kote nchini.

Utekelezaji wa miradi hiyo inayohusisha uimarishaji wa Gridi Imara ya Taifa na usambazaji wa umeme katika maeneo ya vijiji, ni mikakati ya serikali ya kuhakikisha kuwa tatizo la umeme nchini linapatiwa ufumbuzi.

“Miradi hii ina maana kubwa sana kwa wananchi hasa vijijini na taifa kwa jumla, ndiyo maana inapelekwa katika maeneo ya madini, kilimo, viwanda vidogovidogo na vituo vya afya. Ukitaka kuwasaidia wanyonge, wafanyie mambo yao yawe mazuri na ndicho tunachokifanya,” alisema Rais Dk. Samia.

Alisema lengo lingine la kusambaza umeme huo ni kusaidia mkakati wa serikali kuendesha kilimo cha umwagiliaji utakaofanywa na vijana chini ya Mpango wa Kilimo Biashara.

Alisema hatua hiyo itaongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo na hivyo kuliwezesha taifa kuondokana na tatizo la chakula na kwamba uimarishaji wa gridi utaondoa kero ya umeme kukatikatika mara kwa mara.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, awamu ya kwanza ya mkakati huo, itagharimu Sh. trilioni 1.9 ambazo alisema sehemu kubwa ya fedha hizo ni za serikali na nyingine ni za washirika wa maendeleo.

Mradi wa JNHPP, unategemewa kuzalisha megawati 2,115 za umeme utakapokamilika.

Ujenzi wa bwawa hilo umefikia asilimia 83.3 na kina cha maji kimefikia urefu wa mita 135.

Mradi wa JNHPP unaoshika nafasi ya kwanza kwa ukubwa katika miradi yote inayotekelezwa katika nchi za Afrika Mashariki na ni wa nne kwa miradi yote inayotekelezwa Afrika.

Mradi unaoshika nafasi ya kwanza Afrika ni wa Grand Ethiopian Renaissance Dam (6,400 MW) uliopo nchini Ethiopia, namba mbili ni ule wa Batoka George Hydroelectric Dam (2,400 MW), wa nchini Zambia katika Mto Zambezi na wa tatu ni mradi wa Caculo Cabaco Hydroelectric Dam (2,172 Mw) wa nchini Angola.

Gharama za mradi huu wa Bwawa la Nyerere hadi utakapokamilika ni zaidi ya Sh. trilioni 6.5 na tayari mkandarasi ameshalipwa asilimia 65 ya kiasi hicho.

Desemba 22, mwaka jana, Rais Samia alizindua rasmi ujazaji wa maji katika bwawa hilo lenye ukubwa wa kilometa 915 za mraba.

Pia Rais Samia aliwezesha kufanyika kongamano la nishati safi, lililowaleta pamoja watu zaidi ya 300 na kujadili namna nchi itaweza kukakabili matumizi ya nishati chafu.

Aidha, Rais Samia alikuwa mmoja wa walioshiriki mkutano wa wakuu wan chi kuhusu mabadiliko ya tabia nchi (COP27) uliofanyika Afrika kwa mara ya kwanza, akieleza namna Tanzania imeathiriwa na mabadiliko ya tabia nchi huku akizitaka nchi zilizoendelea kulipa fidia kwa nchi maskini.

# Chongolo asema mabosi wazembe watakaa kando

**Na Augusta Njoji,** BABATI

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo amesema chama hicho kinataka ahadi zilizoahidiwa kwa wananchi zitekelezwe kwa vitendo na yeyote atakayekwamisha, atawekwa pembeni.

Pia amelazimika kumwita Waziri wa Maji, Jumaa Aweso mkoani Manyara ili kujibu masuala ya maji mkoani humo ikiwamo mgogoro wa Ayalagaya.

Ni hatua anayoichuku siku chache, kutimiza ahadi yake ya kuwaweka kitimoto viongozi wakuu wa kiserikali, wakiwamo mawaziri.

Akihitimisha jana ziara ya siku sita mkoani Manyara iliyolenga kukagua utekelezaji wa ilani ya CCM 2020-2025, Chongolo alisema suala la umeme lilisuasua awali na wamekubaliana na Wizara ya Nishati ifikapo juni 30 mwaka huu vijiji vyote viwe na umeme na CCM haitahitaji hadithi kwenye hilo.

"Tumekubaliana baada ya kumaliza vijiji vyote hadi Juni mwakani wafikishe umeme kwenye vitongoji vyote. Mtu atakayetukwamisha tutamweka pembeni ya reli ili tuchukue mtu ambaye ataendelea na safari," alisema.

Kuhusu maji, Chongolo alisema kwenye ziara yake limekuwa na malalamiko, hivyo ameona amlete waziri huyo ili kutoa majibu hususan wananchi wa Ayalagaya waliomsimamisha na mabango wakitaka wahudumiwe na Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) na si Mamlaka ya Majisafi Mji wa Babati (BAWASA).

"Nilimwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuwa namtaka waziri wako haraka haraka aje atoe majibu ya malalamiko ya maji ikiwamo suala la Ayalagaya," alisema.

Alipongeza serikali kwa kuleta fedha nyingi za kutatua kero za wananchi Manyara kwenye sekta ya afya, elimu, umeme na maji.

Alisema kuna maeneo yanayohitaji fedha za kusogeza huduma kwa wananchi na atahakikisha zinapelekwa haraka.

Aliahidi kukaa na Rais kumweleza umuhimu wa kupeleka watumishi wa afya kwenye miundombinu mipya ya afya iliyojengwa nchini.

Kuhusu sekta ya elimu, Chongolo alisema kutokana na utekelezaji wa elimu bila malipo inahitaji serikali kupanua wigo wa kupokea wanafunzi wanaofaulu kidato cha tano na sita.

"Nimezungumza na Waziri wa TAMISEMI kuanzia mwezi Aprili mwishoni mwaka huu wataanza kutoa fedha za ujenzi wa madarasa ya kidato cha tano na sita," alisema.

Alitoa wito kwa wananchi wa mkoa huo kuwapeleka watoto kusoma ufundi ambao utatafsiri ajira za moja kwa moja kwa vijana kutokana na miradi mbalimbali inayotekelezwa kuhitaji nguvu kazi yenye ujuzi.

Pamoja na hayo, alisema suala la mashamba ya ngano Basotu, tayari Msajili wa Hazina ameanza mchakato wa kuyapeleka Wizara ya Kilimo ili yatumike.

Akizungumzia vitendo vya ukatili wa kijinsia, Chongolo alisema inahitajika wajifanyie tathmini kutokana na kusikika kwa sifa mbaya ya kuwa mkoa wa pili kwa wingi wa vitendo hivyo.

"Lazima viongozi wa dini, kisiasa na serikali wasimame na kusema kwa uwazi na wale waliopewa dhamana kisheria wasione aibu kuchukua hatua kwa wanaofanya vitendo hivyo na hili pia kwa Mkoa wa Iringa lifanyike wenyewe ndio unaongoza, umeshika nafasi ya kwanza," alisema.

Kuhusu miundombinu ya barabara, Chongolo alisema amechukua kero za barabara na atafikisha kwa Rais Samia kutokana na hali aliyoshuhudia.

Akitoa majibu, Waziri Aweso alisema Babati Mjini mahitaji ya maji ni lita milioni 34 huku mamlaka ikiwa na uwezo wa kuzalisha lita milioni 12 na serikali imeelekeza fedha Sh. bilioni 12 kwa ajili ya mradi wa maji wa Singu utakaozalisha lita milioni 40 ambao ujenzi umefikia asilimia 80.

"Eneo la Ayalagaya wanataka huduma yao itolewe na RUWASA na si BAWASA kutokana na maelekezo ya Rais eneo hili linakwenda kuhudumiwa rasmi na RUWASA," alisema.

Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Sophia Mjema alisema zaidi ya Sh. bilioni 175.7 zimeelekezwa kwenye miradi mkoani humo huku akisisitiza viongozi wa serikali kuitangaza na kuisemea miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yao.

Katibu wa NEC Organizesheni, Issa Haji Gavu alisema CCM itaendelea kusimamia kwa nguvu serikali zote mbili ili zitimize ahadi kwa vitendo huku akisema wameridhishwa na kasi ya utekelezaji wa ilani.

Mwenyekiti wa wabunge wa CCM mkoani Manyara, Christopher Ole Sendeka alisema ziara ya Chongolo imetoa maelekezo mbalimbali kwa serikali na yamezaa matunda kwa wananchi ikiwamo miundombinu ya barabara.

# Mhasibu wa benki atekwa, auawa kwa kuchomwa moto

**Na Waandishi Wetu**

MHASIBU wa Benki ya BOA wilayani Kahama mkoani Shinyanga, Matha Towa (30), amefariki dunia baada ya kutekwa na watu wasiofahamika kisha kuchomwa moto kwa kutumia mafuta yanaodhaniwa ni petroli wilayani Kibaha Mkoa wa Pwani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo aliambia Nipashe jana kuwa tukio hilo lilitokea Machi 3 mwaka huu, maeneo ya Mitamba mkoani Pwani baada ya wasamaria wema kulijulisha Jeshi la Polisi kuhusu tukio hilo.

Alisema wasamaria wema walimkuta Martha, ambaye ni mkazi wa Kwa Mbonde wilayani Kibaha, akiwa na majeraha ya moto na kutoa taarifa polisi majira ya saa 4:30 usiku na polisi walikwenda na kumchukua kisha kumpeleka Hospitali ya Mkoa wa Pwani (Tumbi), Kibaha.

Alisema kuwa baadaye alihamishiwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa matibabu zaidi na usiku wa kuamkia juzi (Machi 9) alifariki dunia.Kamanda Lutumo alisema kutokana na mazingira yenye utata ya kifo hicho, Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi ikiwako kubaini sababu za kuchomwa moto.

Wakati hayo yakiendelea Kibaha, tukio lingine la mauaji limeripotiwa mkoani Tabora, Salima Maulid (34) akidaiwa kuuawa na mume wake kisha kufukiwa kwenye chumba walichokuwa wanalala kwa madai ya wivu wa mapenzi.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, Richard Abwao, akizungumza na waandishi jana, alisema tukio hilo lilitokea Machi 7 mwaka huu.

Alisema mwanaume huyo ambaye kwa sasa anatafutwa baada ya kukimbia, alipomuua mke wake, alichimba shimo kisha kumfukia na kusakafia kwa zege na kuweka kitanda juu yake.

Akisimulia zaidi kuhusu tukio hilo, Kamanda Abwao alisema lilitokea majira ya saa 9.30 alasiri kwenye Mtaa wa Mbilani, Kata ya Kidongo Chekundu, Manispaa ya Tabora.

Alisema Michael Hendry baada ya kuona siku kadhaa zimepita bila chumba hicho kufunguliwa, walilazimika kuvunja mlango wa chumba cha kulala na kukuta chini ya kitanda kuna zege likiwa halijakauka vizuri.

"Baada ya kuona hivyo, alipata hofu ndipo walipoamua kufukua eneo hilo na kukuta mwili wa mtu umefukiwa kwenye shimo hilo. Chanzo cha kifo hicho ni wivu wa mapenzi," alidai.

Kamanda alisema mtuhumiwa baada ya kutekeleza unyama huo, alikimbia na jitihada za kumtafuta zinaendelea.

Alisema Jeshi la Polisi linawataka wananchi ambao wanafahamu mtuhumiwa huyo aliko, watoe taarifa.

***Imeandaliwa na Julieth Mkireri (KIBAHA) na Halima Ikunji (TABORA)**

## Majaliwa: Ukatili mtandaoni unawanyima fursa wanawake

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema mabadiliko ya kidijitali katika uchumi, yamesababisha kuongezeka kwa unyanyasaji na ukatili wa kijinsia mtandaoni.

Amesema hali hiyo inawafanya wanawake wengi kuacha kushiriki na kuwanyima fursa mbalimbali zilizopo mitandaoni.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati Mkutano Mkuu wa Tano wa Mwanamke Kiongozi Mwaka 2023 uliofanyika sambamba na mahafali ya wahitimu 67 wa Awamu ya Nane ya Mafunzo ya Mwanamke Kiongozi inayoratibiwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE).

Majaliwa alisema anatambua kuwapo vikwazo mbalimbali vinavyopunguza ushiriki wa wanawake katika kushiriki fursa za kidijitali kama vile kukosa maarifa na ujuzi wa namna ya kushiriki, kumudu gharama za data na vifaa vinavyowaunganisha na ulimwengu.

"Changamoto hizi ni mtambuko, hivyo zinahitaji ushiriki wa wadau mbalimbali katika kuhakikisha kuwa wanawake wanaweza kushiriki kwa ukamilifu fursa hizi na kuongeza ukuaji wa uchumi.

"Na katika hili ninaipongeza ATE kuleta mjadala huu katika mkutano huu wa leo (jana) na ninaamini mtatoka na maazimio na mikakati muhimu ya kukabiliana na changamoto hizo," alisema.

Pia alisema suala la shambulio la kimtandao (cyber attacks) limeendelea kuwa tishio na serikali kwa kutambua hilo, imeendelea kuimarisha usalama wa mtandao kwa kuwajengea uwezo wataalamu wa ndani wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

"Nitoe rai kwa ATE kuendelea kuwasisitiza waajiri kuboresha mifumo yao ya kidijitali na kuona ni namna gani wanawaelimisha wafanyakazi wao kuhusu matumizi sahihi na chanya ya dijitali," aliagiza.

Majaliwa aliwataka wanawake wajitokeze kwa wingi kushiriki katika programu hiyo ya mafunzo ATE kwa kuwa imeendelea kuwa na matokeo chanya kwa washiriki na kuleta mabadiliko makubwa kwenye utendaji wao wa kazi na kugusa maisha yao binafsi.

"ATE mwendelee kutoa mafunzo haya na kuendelea kuwa vinara katika kuhakikisha usawa wa kijinsia unafikiwa maeneo ya kazi.

"Ninazihimiza kampuni kutunga sera zinazojali usawa wa kijinsia na kuhakikisha wanawake wanapewa kipaumbele katika uongozi ili kuwapa nafasi ya kushiriki kutoa maoni na uamuzi," alielekeza.

Mtendaji Mkuu wa ATE, Suzanne Ndomba-Doran alisema wanaamini mabadiliko ya kidigitali yameleta matokeo makubwa katika ulimwengu wa kazi, kipindi cha UVIKO-19 wengi walitegemea teknolojia kuendeleza biashara na shughuli za kiuchumi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako alisema wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO), ATE na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), wameendelea kufanya kazi kwa pamoja kwenye maeneo kama afya na usalama mahali pa kazi.

# HADITHI

# MTAKE MSITAKE-22

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa kiburi baadhi ya viongozi wa kijiji kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji na kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yanayopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, mmoja ya wasichana warembo kijijini hapo ni mmoja ya waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**




Jaribio alilokuwa analifanya la kutaka kumlazimisha Adel kuondoka jijini hapo, au kumteka lisingefanikiwa kamwe kwa sababu hakuwa raia wa kawaida. Alikuwa ni mtu wa usalama aliyeletwa hapo kufanya kazi hiyo. Angeweza kuwamaliza wote kabla hawajafanya chochote. Makao Makuu hawakutaka ajiingize kwenye masuala hayo kabla kazi mama haijafanyika. Hawakutaka Adel ajulikane kuwa si mtu wa kawaida. Chochote ambacho angekifanya kwa waliotaka kumteka kwa sababu ya kuonekana kuwa na Mary, kingeweza kuwashtua wanakijiji na wengine, hivyo mpango ukaharibika. Sasa mambo yamekwisha.

"Kitu cha mwisho nataka niwaambie." Akasema na kuwafanya watu wanyamaze na kutaka kumsikiliza tena kwani vitu anavyoongea vingi walipenda kuvisikia na vilikuwa ni vya kushangaza na kufurahisha kwa upande wao.

"Hili hata mimi limenishangaza. Nilichokuja kugundua baadaye kumbe Enock si mpenzi wa Mary kama wengi walivyokuwa wanaona au kudhania kwenye kijiji hiki." Mshtuko tena uliwapata wanakijiji. Wanachofahamu siku zote ni kwamba Enock aliachana na Amina halafu akawa na Mary. Leo huyu ambaye amekuja tu kwenye kijiji anakuja kusema hawa si wapenzi. Kwa sababu tayari wameshafahamu kuwa ni mpelelezi, mtu wa usalama, walimsikiliza ili wajue ni kwa nini? Kitu gani amekiona hadi anawathibitishia kuwa Enock na Mary si mtu na mpenzi wake?

"Ni hivi. Usonzo alipoingia kwenye hiki kijiji na kuingia mikataba yake feki, alibahatika kumuona binti huyu na kumtongoza. Binti akakataa. Alipokataa akamtisha kuwa atamfanyizia. Hilo lilimtisha sana binti huyo, na kwenda kushtaki kwa wazazi wake. Kwa jinsi alivyochukua ardhi yao, wazazi wa Mary walijua kabisa kuwa kwa vyovyote hawatoweza kumfanya kitu chochote Usonzo kama akiamua kufanya lolote. Na kwa sababu Mary hakuwa hasomi, hata mume, mchumba wala mpenzi, kingeweza kufanyika kitu chochote kile na Serikali ya Kijiji isichukue hatua yoyote. Walichofanya ni kwenda kuongea na Enock ambaye kwa mbali kidogo ana undugu na Mary. Ukatengenezwa uchumba ambao haukuwa kweli, lakini ukapata baraka zote kutoka kwa ndugu wa karibu ili kumlinda Mary.

**"Samahanini sana, nimechelewa sana, unajua tena, unakwenda huko unakutana tena na watu wengine wenye shida zao."**

Hii kidogo ilisaidia kwani Usonzo pamoja na mambo yake yote, lakini alikuwa akiingia anapotambua kuwa msichana huyo ana mchumba wake. Vinginevyo hali ingekuwa mbaya sana. Hata mzee Chale Mwenyekiti wa Kijiji alikuwa akimuonya Usonzo kuwa japo ameinunua ardhi, lakini ajaribu kuheshimu utamaduni wa kijiji, na mara kwa mara alikuwa akimuonya kuhusu msichana Mary, ingawa baadaye alianza kubadika baada ya mimi kuingia kwenye kijiji hiki na kuniona nikiwa naye. Ilikuwa inamuuma sana na akaanza tena kumfuatilia na kumuuliza kwa nini amekuwa na uhusiano na mimi na kumuacha yeye. Na Usonzo alikuwa akiumia sasa kwa sababu yeye alikataliwa ya kuambiwa ana mchumba ambaye ni Enock, sasa akawa anamuuliza kwa nini umemkubalia Adel wakati pia una mchumba?"

Tayari kila kitu kilikuwa hadharani. Kijiji kilifahamu kuwa uchumba wa Enock na Mary ulikuwa ni wa kutengeneza. Ulikuwa ni kinga kwa Mary ili Usonzo asimfanyie unyama, aogope kwa sababu tayari msichana huyo ana mtu.

"Nadhani tumeshamaliza. Kila kitu kiko tayari. Usonzo na mzee Chale watapelekwa Dar es Salaam, ushahidi kila kitu nimeshawakabidhi wenzangu. Na mimi tu niwaambie, hawa wataondoka leo. Lakini na mimi tayari nimeshamaliza kazi yangu. Nitaondoka kesho kutwa kurudi kwetu."

Adel alisikia sauti za "aaa, kaa na sisi, tutakupa cheo. Uwe mwenyekiti wetu." Ilisikika moja kati ya sauti nyingi zilizosikika kutoka kwa umati wa wanakijiji.

"Nashukuru sana kwa kutaka kunipa cheo, au kutaka kunichagua. Kama mlivyosikia mimi ni mtu wa usalama, na hapa nimekuja kufanya kazi hii tu. Lakini kwa sababu ya aina ya kazi niliyoifanya, nakuhakikishieni nitakuwa nanyi pamoja. Nikisema nitakuwa nanyi pamoja nina maana pana sana. Kuanzia leo niwaambie tu mimi ni shemeji yenu."

Zilisikika shangwe kutoka kwa umati ule hasa kinamama ambao walianza kupiga vigelegele na kuimba.

"Ngojeni kwanza, mbona mnaimba na vigelegele wakati hamjajua nini nataka kusema?"

"Tunajuaaa" zilisikika sauti.

"Mnajua nini?"

"Mary"

Adel akaangua kicheko, akakohoa, halafu akaendelea.

"Ni kweli, kuanzia leo nawatangazia rasmi kuwa mimi ni mchumba wa Mary. Nilianza kumpenda tangu siku ya kwanza nilipomuona kwenye mkutano wa kijiji. Na hata siku niliyokutana naye mara ya pili na kumuokoa kwenye ajali ya pikipiki. Ingawa ni msiri, alianza kwa kunikataa, akaniambia kweli unanipenda, lakini nina mchumba anaitwa Enock. Kitu ambacho kilimfanya kuniambia siri yake kuwa Enock hakuwa mchumba halisi ni pale alipoona pamoja na kukataliwa, bado niliendelea kumpenda, kuwasiliana naye na sikuonyesha kukasirishwa kwa namna yoyote ile, au kumuacha na kuanza kufuata wanawake wengine ambao hawana wapenzi. Akanikutanisha na Enock. Kumbe ulikuwa ni mpango wao tu wa kuniweka karibu. Niliposikia kuwa hakuwa mpenzi wake kwanza sikuamini, halafu Enock mwenyewe akasema yeye anajivua, kwani Mary sasa amepata mpenzi halisi na yeye akarejea kwa mpenzi wake Amina. Nikamwambia kwanza endelea kwa sababu kuna mpango nataka kuufanya. Ikawa ni timu ya watu watatu. Nikawaambia na mimi kazi yangu niliyojia kwenye kijiji hicho, hapo ndipo tulipotengeneza mkakati huu uliofanikiwa kwa asilimia 100."

Wengine sasa hawakutaka kusikia chochote walikuwa na shangwe tu ya kuwa huru, ardhi yao imerudi, kumbe Adel si kipofu, kumbe Adel ni mpelelezi aliyekuja kukirudisha kijiji mikononi kwa wananchi, halafu pia Enock si mchumba wa Mary na sasa kumbe Adel ndiye anakuwa mchumba halisi wa Mary.

"Naomba Mary usimame uje kwenye jukwaa hapa, uongee mawili matatu, halafu nikupe zawadi yako, ambayo itawatambulisha watu wote hapa kuwa mimi na wewe ni wachumba na hanitaji uwe mke wangu."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# NBC YAKABIDHI FEDHA, TUZO KWA KOCHA MECKY MAXIME

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) ambayo ni mdhamini Mkuu wa Ligi Kuu ya soka Tanzania Bara, juzi ilikabidhi zawadi ya fedha na tuzo kwa kocha bora wa mwezi wa ligi hiyo, Mecky Maxime kutoka klabu ya Kagera Sugar.

Makabidhiano ya zawadi hizo yalifanyika muda mfupi kabla ya kuanza kwa mchezo baina ya KMC FC na Kagera Sugar uliofanyika katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

**Tuzo hiyo ilikuwa ya kocha bora wa Februari na mchezo huo ulimalizika kwa KMC FC kuibuka na ushindi wa mabao 2-0.**

Tukio la makabidhiano ya zawadi hizo, lilishuhudiwa na Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa wateja, Salama Mussa ambaye alikabidhi mfano wa hundi ya fedha yenye thamani ya Sh Milioni moja pamoja na tuzo kwa kocha Maxime.

"Benki ya NBC kwa kiasi kikubwa tunaridhishwa na kasi ya ushindani inayoendelea kwenye ligi ya NBC," alisema Salama.

Aliongeza; "Zaidi pia tunafurahishwa kuona mchezo huu unavyochochea ajira nyingine zisizo za moja kwa moja ikiwemo wafanyabiashara ndogo ndogo na kubwa wanaonufaika kupitia mauzo ya bidhaa mbalimbali zinazohusisha mchezo huu zikiwemo jezi, huduma za vyakula na vinywaji kwa timu na mashabiki."

Aidha Salama alitoa wito kwa mashabiki wa mchezo huo kujitokeza kwa wingi kwenye viwanja mbalimbali ambavyo michezo ya ligi hiyo inaendelea ili kufurahia na kuhamasisha timu zao ziweze kufanya vizuri zaidi na kuleta ushindani unaotakiwa.




Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa wateja wa Benki ya NBC, Salama Mussa (kushoto) akikabidhi mfano wa hundi ya fedha yenye thamani ya Sh milioni moja pamoja na tuzo kwa kocha bora wa mwezi wa ligi Kuu Tanzania Bara, Mecky Maxime wa Kagera Sugar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Serikali kutoa tuzo za wanamichezo Machi 17*

**Na Saada Akida**

WIZARA ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na Baraza la Michezo Taifa (BMT), imeandaa tuzo ya wanamichezo bora inayotarajiwa kufanyika Machi 17, Mwaka huu, Mlimani City, Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa BMT, Leodger Tenga alisema dhamira ya hafla ni kuwaenzi na kuwaheshimisha wanamichezo kwa kufanya vizuri katika michezo ya Kanda, Afrika na michuano ya kimataifa.

Alisema wamedhamiria mwaka huu kutoa nishani, stashahada, vyeti, makombe na vivutio vingine baada ya kushirikiana na vyama vya kitaifa kwa ajili ya kuhimiza na kukuza shughuli za michezo nchini.

"BMT inaona sasa ni wakati muafaka kuanza kutambua na kuwapongeza wanamichezo na timu za kitanzania zinazofanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya kimataifa na kuitangaza nchi yetu," alisema Tenga.

Alisema Tuzo hizo zimewazingatia waliofanya vizuri mwaka jana na lengo kubwa kutambua, kuwaenzi na kuwapongeza wanamichezo ili kuleta hamasa kwa vijana ambao hawakupata nafasi ya kufanya vizuri.

Tenga alisema kuanzia mwaka huu tuzo hizo zitakuwa na vipengele nane ambavyo ni mwanamichezo bora wa kiume na kike, mwenye ulemavu kwa jinsi zote mbili, mwanamichezo bora wa kike na kiume katika michezo ya shule, timu na wanamichezo bora zilizofanya vizuri katika mashindano ya kimataifa.

"Katika kuhakikisha mchakato wa utoaji tuzo unafanyika kwa wazi, weledi na umakini mkubwa vyama na mashirikisho yote ya michezo yameshirikiana katika uteuzi wa wanamichezo bora katika michezo yao," alisema Tenga.

Alisema vipengele vya wanamichezo bora kwa jumla, kamati ya usimamizi wa tuzo za michezo itachagua majina ya wanamichezo watatu kutoka kwenye orodha iliyowasilishwa na vyama vya michezo kwa kamati ya jopo la majaji ambao watachambua majina hayo na kuchagua wanamichezo bora kwa jumla katika vipengele husika.

Kamati hiyo inaongozwa na Mwenyekiti Mkumbukwa Mtambo, Leonard Thadeo (Makamu Mwenyekiti), Neema Msitha (Katibu), Wajumbe ni Jonas Tiboroha, Nasra Mohammed, Christiana Kokomo, Boniface Wambura na Kanali Mstaafu Juma Ikangaa na Omar Omar.

## Polisi yalia na usajili mbovu

**Na Hadija Mngwai**

TIMU ya Polisi Tanzania imeeleza kuwa, kufanya makosa katika dirisha kubwa la usajili lililopita ndio kumeisababishia kuwa katika hali mbaya kwenye Ligi Kuu Tanzania msimu huu.

Polisi ipo nafasi ya 15 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa imecheza mechi 24 ambapo imebakiza michezo sita ikiwa katika hatari ya kushuka daraja iwapo itamaliza Ligi Kuu katika nafasi hiyo.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Habari wa Polisi, Frank Rukwalo amesema kuwa, timu yao imeyumba na kutofanya vizuri kutokana na usajili mbovu walioufanya mwanzoni mwa msimu kabla ya kufanya maboresho katika dirisha dogo.

"Unajua ukishakosea tu kwenye usajili mwanzoni mwa msimu hali inakuwa tofauti ndio jambo lililopelekea timu yetu kuwa katika hali hii," alisema.

Aliongeza; "lakini tumeshafanya marekebisho kwenye usajili wa dirisha dogo lililopita tumeongeza maingizo mapya, tunaamini tutafanya vizuri katika mechi sita zilizobakia.

## Singida Big Stars yaipania Coastal Union

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Singida Big Stars imejipanga kufanya vizuri zaidi kwenye mchezo wake wa kesho Jumapili dhidi ya Coastal Union kwenye uwanja wa Mkwakwani, Tanga

Akizungumza na Nipashe, Kocha Mkuu wa Singida Big, Stars Hans Van Pluijm alisema wachezaji wake wanaendelea vema na wapo tayari kwa mchezo huo.

"Tunaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wetu dhidi ya Coastal Union, tunafahamu utakuwa mgumu kwani kila timu inahitaji pointi tatu, lakini tumejipanga vyema kabisa," alisema Pluijm.

Kocha huyo alisema mchezo huo unatarajiwa kuwa mgumu na wenye upinzani na kudai Ligi Kuu msimu huu ina ushindani mkubwa.

Aidha alisema mchezaji wake Bruno Gomes kwa sasa anaendelea vizuri na kuomba mashabiki wao waendelee kuwapa ushirikiano.

Alisema anashukuru wachezaji kutokana na nidhamu wanayoionesha nje na ndani ya uwanja ambayo inawapa mafanikio ndani ya timu yao hiyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

**HAALAND ATAKIWA MADRID**
REAL Madrid wanafikiria kumnunua mshambuliaji wa Manchester City na Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 22 msimu wa joto kama sehemu ya mpango wa kuleta kizazi kipya cha nyota wachanga ambao pia ni pamoja na kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19. (***Independent***)

**MAGUIRE PAUNI MIL 50**
MLINZI wa Manchester United na England, Harry Maguire mwenye umri wa miaka 30, anawaniwa kwa pauni milioni 50 na Paris St-Germain msimu wa joto. (***Sun***)

**KANE HATAKIWI BAYERN**
RAIS wa heshima wa Bayern Munich, Uli Hoeness amesema "itakuwa jambo la kustaajabisha" ikiwa mabingwa hao wa Ujerumani watamnunua mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane mwenye umri wa miaka 29, na kwamba siku ambayo klabu hiyo itatumia euro milioni katika uhamisho "inakuja". (Sky Sport Germany)

**MOUNT AWINDWA MAN**
KLABU ya Manchester United imemuongeza kiungo wa kati wa Chelsea na England, Mason Mount mwenye umri wa miaka 24, kwenye orodha ya wachezaji wanaotarajiwa kusajiliwa msimu wa joto. {***Guardian***)

**POCHETTINO KURUDI SPURS**
MAURICIO Pochettino ameiambia Tottenham Hotspur kwamba ana nia ya kurejea na kuchukua nafasi ya Antonio Conte kama kocha, lakini Muargentina huyo mwenye umri wa miaka 51 pia ana chaguo kutoka kwa klabu za nje ya England. (***talkSPORT***)

**CONTE KUTIMULIWA**
KLABU ya Tottenham Hotspur itajadili sifa za Mauricio Pochettino na Thomas Tuchel kama wasimamizi wanaoweza kurithi nafasi ya Antonio Conte, ambaye klabu hiyo imepanga kuachana naye. (***Guardian***)

**WATANO WATAJWA**
KOCHA wa Brentford, Thomas Frank na Marco Silva wa Fulham pia wako kwenye orodha ya makocha watano wanaowaniwa kuteuliwa kuchukua nafasi ya Antoni Conte pale Tottenham. (Independent)

**LAPORTE KUUZWA**
KLABU ya Manchester City iko tayari kumuuza mlinzi wa Hispania, Aymeric Laporte mwenye umri wa miaka 28 msimu huu wa joto ikiwa klabu hiyo inaweza kupata mchezaji wa kiwango cha juu. (***Football Insider***)

**DYBALA KUTUA MAN**
MANCHESTER United ni moja ya klabu zinazovutiwa na mshambuliaji wa Argentina, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 29, ambaye anaweza kusajiliwa kwa pauni milioni 11 msimu wa joto licha ya kujiunga na AS Roma mwaka jana. (***Goal***)

**RAYA KUONDOKA BRENTFORD**
KLABU ya Manchester United pia imejiunga na orodha inayovutiwa na mlinda mlango wa Brentford, David Raya, huku Mhispania huyo mwenye umri wa miaka 27 akitarajiwa kuondoka kwa Nyuki hao baada ya kukataa mkataba mpya. (***talkSPORT***)

**BARCA YAMTAKA CANCELO**
MLINZI wa pembeni wa Manchester City na Ureno, Joao Cancelo mwenye umri wa miaka 28, ameibuka kama mchezaji anayelengwa na Barcelona mara muda wake wa mkopo kule Bayern Munich utakapokamilika msimu wa joto. (***Sport***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# DE JONG ATANGAZA HAONDOKI BARCELONA

**BARCELONA,** Hispania

## Asema anataka kushinda taji la LaLiga na Wakatalunya hao huku mkataba wake...

FRENKIE de Jong ametangaza kuwa hana nia ya kuondoka Barcelona huku kukiwa na taarifa ya kuhusishwa na Manchester United.

Kiungo huyo wa kati mwenye umri wa miaka 25 alihusishwa kwa kiasi kikubwa kuhamia Old Trafford katika msimu uliopita, lakini haikuwezekana licha ya juhudi kubwa za kocha wa United, Erik ten Hag kumshawishi.

Hali hiyo ilitatizwa na hali ya kimkataba ya De Jong na Barcelona ambayo ina matatizo ya kifedha, na hivyo kugeuka kuwa sakata la muda, na hivyo kuzua gumzo kwamba United inaweza kumnunua tena mwishoni mwa msimu huu.

Lakini De Jong ameweka wazi kuwa hana nia ya kuondoka hapo Camp Nou, ambako ana mkataba hadi mwaka 2026.

"Nilikuwa mtulivu kwa sababu nilijua nilitaka kubaki Barca na sijabadilisha mawazo yangu," alisema De Jong akiiambia RAC1.

"Siku zote nilikuwa na ndoto ya kuichezea Barcelona na ninataka kufanikiwa Barca. Kwa sasa nimetulia na nataka kuendelea Barca."

De Jong, ambaye alijiunga na Barcelona kutoka Ajax mwaka 2019, aliongeza kuwa alikuwa na mengi ya kufanikiwa akiwa na Wakatalunya hao. "Sijawahi kushinda Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga," alisema. "Ni mwaka wangu wa nne hapa na ni wakati ambao nimekuwa karibu zaidi. Lakini bado kuna safari ndefu.

"Ni lengo letu kuu na tutatoa kila kitu ili kufikia hilo."

De Jong ameanza mara 18 akiwa amecheza mechi nne akitokea benchi katika michezo 24 za Barcelona za LaLiga msimu huu, na kuhakikisha amekuwa sehemu muhimu ya mafanikio yao, huku wakiongoza msimamo wa pointi tisa zikiwa zimesalia mechi 14 Ligi kumalizika msimu huu.

"Mfumo wa viungo wanne unaninufaisha, lakini zaidi ya hapo, mwaka huu nacheza zaidi kwenye safu ya kiungo, ambapo najisikia raha zaidi," alisema.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,087,3

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 14,15 NA 16 MACHI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/03/23 | 23:00 | Porto vs Inter | 2.60 | 3.30 | 2.49 |
| 02. 15/03/23 | 02:05 | Tlaxcala FC vs Venados FC | 2.58 | 3.15 | 2.53 |
| 03. 15/03/23 | 04:10 | Independiente Santa Fe vs America De Cali | 2.27 | 3.06 | 3.01 |
| 04. 15/03/23 | 06:05 | Correcaminos Uat vs Tepatitlan FC | 2.24 | 3.11 | 3.01 |
| 05. 15/03/23 | 19:30 | NK Celje vs Olimpija Ljubljana | 2.62 | 3.23 | 2.39 |
| 06. 15/03/23 | 22:30 | Southampton vs Brentford | 2.85 | 3.15 | 2.38 |
| 07. 15/03/23 | 23:00 | Real Madrid vs Liverpool | 2.33 | 3.46 | 2.68 |
| 08. 16/03/23 | 20:45 | Fenerbahce vs Sevilla FC | 2.23 | 3.37 | 3.16 |
| 09. 16/03/23 | 20:45 | Djurgardens IF vs Lech Poznan | 2.46 | 3.27 | 2.72 |
| 10. 16/03/23 | 20:45 | Slovan Bratislava vs FC Basel | 2.47 | 3.23 | 2.73 |
| 11. 16/03/23 | 23:00 | AZ Alkmaar vs Lazio | 2.83 | 3.28 | 2.37 |
| 12. 16/03/23 | 23:00 | Union Saint Gilloise vs Union Berlin | 2.77 | 3.32 | 2.39 |
| 13. 16/03/23 | 23:00 | Real Sociedad vs Roma | 2.19 | 3.27 | 3.32 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa · vodacom m-pesa · halopesa · airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# RASHFORD AKUNWA NA KIWANGO CHA MAN UNITED KWA BETIS

**MANCHESTER,** England

MARCUS Rashford alifurahishwa na ushindi wa Manchester United kwenye Ligi ya Europa dhidi ya Real Betis Alhamisi baada ya kukutana na kichapo cha fedheha kutoka kwa Liverpool.

Kikosi cha United ambacho hakikubadilika na kile kilichofungwa kule Anfield Jumapili, kiliibuka na ushindi wa 4-1 kwenye uwanja wa Old Trafford kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya 16 bora.

Rashford alitangulia kufunga, huku Antony, Bruno Fernandes na Wout Weghorst kila mmoja akifunga bao katika kipindi cha pili baada ya Ayoze Perez kuwasawazishia wageni.

Ingawa ushindi huo hautaondoa maumivu waliyopata kule Merseyside, uliirudisha United kwenye mstari na Rashford amesema kuna zaidi yanayokuja.

"Siku zote ni muhimu kushinda mechi inayofuata, ndiyo njia pekee ya sisi kurejea na kujaribu kuendeleza kasi tuliyokuwa nayo kabla ya mchezo huo," alisema akiiambia BT Sport.


"Kwa hiyo nimefurahi tumefanikiwa kushinda mchezo huo na imetuweka katika hali nzuri kwenye sare.

"Siku zote tunajaribu kuanza haraka, bao huwa linasaidia sana. Nilidhani walilinda eneo la hatari katika kipindi cha kwanza, kipindi cha pili kilifunguka zaidi, kama tulivyotarajia mchezo ukiwa 1-1, kwa hiyo nimefurahi kushinda mchezo na kuanza sare kwa njia sahihi.

"Ni hatua ya kurejea katika mwelekeo sahihi, inabidi tujenge kwenye hili sasa ili kupata kasi tena, hatuwezi kuweka mkazo sana kwenye jambo ambalo limepita, hatuwezi kulibadilisha, lakini ni lazima tuangalie mbele sasa."

# Mourinho: Roma bado ina kazi ngumu

**ROME,** Italia



LICHA ya AS Roma kushinda 2-0 dhidi ya Real Sociedad katika mchezo wao wa mkondo wa kwanza wa hatua ya 16 bora wa Ligi ya Europa Alhamisi, lakini kocha mkuu Jose Mourinho alikataa kuyaita matokeo mazuri.

Mabao ya Stephan Al Shaarawy na mchezaji wa akiba Marash Kumbulla yalifanikisha ushindi wa nyumbani ambao unawapa Giallorossi faida kubwa kabla ya mechi ya marudiano mjini San Sebastian.

Licha ya hayo, Mourinho hakuridhika, akihimiza tahadhari kwani hawajajihakikishia kutinga robo fainali.

"Hii 2-0 ni nzuri tu ikiwa hatutapoteza kwenye mchezo wa pili," alisema Mourinho akiiambia Sky Sport Italia.

"Sitawahi kusema ni matokeo mazuri baada ya mechi ya kwanza."

Mourinho alikiri Roma kuwa na ratiba ngumu katika mechi ya mkondo wa pili Alhamisi 16 Machi, na Dabi ya Capitale dhidi ya Lazio siku tatu baadaye.

"Sasa tuna wiki hatari," alisema Mreno huyo.

"Baada ya kurudiana na Real Sociedad tunacheza dhidi ya Lazio, hata kama kwangu kucheza nao ni kama kucheza na Milan au Juve, lakini katika jiji hili si hivyo."

## HABARI MICHEZO


305,640/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/03/23 | 18:00 | Everton FC vs Brentford FC | 2.55 | 3.05 | 2.70 |
| 02. 11/03/23 | 18:00 | Preston North End vs Cardiff City | 2.55 | 3.10 | 2.70 |
| 03. 11/03/23 | 18:00 | Queens Park Rangers vs Watford FC | 2.65 | 3.15 | 2.50 |
| 04. 11/03/23 | 18:15 | Elche CF vs Real Valladolid | 2.65 | 3.15 | 2.55 |
| 05. 11/03/23 | 18:30 | FC Pacos Ferreira vs Santa Clara Azores | 2.31 | 3.15 | 2.95 |
| 06. 11/03/23 | 20:15 | KAS Eupen vs KV Oostende | 2.46 | 3.30 | 2.60 |
| 07. 11/03/23 | 22:45 | Bologna FC vs Lazio Rome | 2.95 | 3.15 | 2.29 |
| 08. 11/03/23 | 23:00 | Sparta Rotterdam vs Vitesse Arnhem | 2.35 | 3.25 | 2.80 |
| 09. 12/03/23 | 14:15 | NEC Nijmegen vs FC Utrecht | 2.45 | 3.20 | 2.70 |
| 10 12/03/23 | 14:30 | US Lecce vs Torino FC | 2.85 | 2.90 | 2.55 |
| 11. 12/03/23 | 16:00 | RCD Mallorca vs Real Sociedad San Sebastian | 3.20 | 2.85 | 2.36 |
| 12. 12/03/23 | 17:00 | AC Ajaccio vs Montpellier HSC | 2.75 | 3.10 | 2.50 |
| 13. 12/03/23 | 17:00 | FC Nantes vs OGC Nice | 3.05 | 3.10 | 2.28 |
| 14. 12/03/23 | 17:00 | Hellas Verona vs AC Monza | 2.36 | 3.05 | 2.95 |
| 15. 12/03/23 | 18:30 | Rio Ave FC vs Gil Vicente Barcelos | 2.28 | 3.10 | 3.05 |
| 16. 12/03/23 | 20:30 | KRC Genk vs Union Saint-Gilloise | 2.29 | 3.40 | 3.05 |
| 17. 12/03/23 | 21:30 | VfL Wolfsburg vs Union Berlin | 2.26 | 3.20 | 3.30 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 11/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1275 | FC Minaj vs Oleksandria | 3.80 | 3.24 | 1.86 |
| 14:00 | 1705 | Torpedo Moscow vs Ural Yekaterinburg | 3.39 | 3.34 | 2.02 |
| 15:15 | 3880 | Hearts vs Celtic | 7.45 | 5.38 | 1.28 |
| 15:30 | 3119 | Bournemouth vs Liverpool | 5.99 | 4.30 | 1.45 |
| 16:00 | 1087 | Chernomorets Odessa vs FC Metalist 1925 | 2.62 | 3.23 | 2.39 |
| 16:00 | 2304 | Mtibwa Sugar vs Simba | 6.07 | 3.37 | 1.21 |
| 16:00 | 2787 | Hapoel Haifa vs Maccabi Tel Aviv | 4.30 | 3.74 | 1.64 |
| 16:00 | 3155 | Real Madrid vs Espanyol | 1.29 | 4.96 | 9.01 |
| 16:00 | 5689 | Antalyaspor vs Kayserispor | 2.20 | 3.31 | 3.05 |
| 16:30 | 1058 | Spartak Moscow vs Fakel | 1.33 | 4.81 | 7.74 |
| 16:30 | 5152 | Akhmat Grozny vs Lokomotiv Moscow | 2.14 | 3.35 | 3.09 |
| 16:35 | 2503 | Masafi vs Fursan Hispania FC | 1.37 | 4.42 | 6.58 |
| 16:35 | 3786 | AL Tawon SC vs AL Urooba | 3.28 | 3.38 | 1.97 |
| 16:35 | 4726 | Masfoot Sports Club vs AL-Rams | 1.41 | 4.23 | 5.99 |
| 16:40 | 3906 | Al-Hamriyah vs City Football Club | 1.26 | 5.13 | 8.20 |
| 16:45 | 3093 | Al Nasr Dubai vs Baniyas | 1.97 | 3.39 | 3.24 |
| 16:45 | 4758 | Jazira Abu Dhabi vs Shabab AL Ahli Dubai Club | 2.71 | 3.32 | 2.27 |
| 17:00 | 1756 | Empoli vs Udinese | 2.84 | 3.19 | 2.36 |
| 17:00 | 2863 | Banik Ostrava vs Sparta Prague | 3.76 | 3.49 | 1.90 |
| 17:30 | 2889 | RB Leipzig vs Monchengladbach | 1.39 | 4.80 | 6.19 |
| 17:30 | 3090 | Bayern Munchen vs Augsburg | 1.15 | 7.09 | 12.97 |
| 17:30 | 5179 | Eintracht Frankfurt vs Stuttgart | 1.78 | 3.60 | 4.00 |
| 17:30 | 5406 | Hertha BSC vs Mainz | 2.79 | 3.29 | 2.33 |
| 18:00 | 1281 | Leeds vs Brighton | 3.55 | 3.45 | 1.93 |
| 18:00 | 3208 | Everton vs Brentford | 2.60 | 3.05 | 2.65 |
| 18:00 | 5659 | Tottenham vs Nottingham | 1.41 | 4.39 | 6.59 |
| 18:00 | 5765 | Leicester vs Chelsea | 3.60 | 3.40 | 1.93 |
| 18:15 | 2978 | Elche vs Valladolid | 2.54 | 3.14 | 2.64 |
| 18:30 | 1404 | Emmen vs SBV Excelsior | 1.73 | 3.59 | 4.29 |
| 18:30 | 2424 | GD Chaves vs Portimonense | 2.23 | 3.22 | 3.07 |
| 18:30 | 4312 | Pacos Ferreira vs Santa Clara | 2.37 | 3.15 | 2.90 |
| 18:30 | 5087 | Hapoel Katamon vs Maccabi Bney Reine | 1.64 | 3.48 | 4.71 |
| 19:00 | 1233 | Namungo vs Tanzania Prisons | 1.77 | 3.13 | 4.41 |
| 19:00 | 4546 | FC Krasnodar vs Dinamo Moscow | 2.66 | 3.29 | 2.43 |
| 19:00 | 5158 | Galatasaray vs Kasimpasa | 1.30 | 5.26 | 7.79 |
| 19:00 | 5402 | AJ Auxerre vs Rennes | 3.66 | 3.31 | 1.94 |
| 19:30 | 2046 | Sectzya Nes Ziona vs Hapoel Hadera | 2.78 | 2.98 | 2.41 |
| 20:00 | 4292 | Arab Contractors vs Smouha Club | 2.31 | 2.85 | 3.31 |
| 20:00 | 4380 | Napoli vs Atalanta | 1.68 | 3.70 | 4.42 |
| 20:30 | 1438 | Schalke 04 vs Borussia Dortmund | 4.21 | 3.86 | 1.68 |
| 20:30 | 3110 | Celta Vigo vs Rayo Vallecano | 2.03 | 3.09 | 3.64 |
| 20:30 | 5097 | Crystal Palace vs Manchester City | 7.27 | 4.38 | 1.38 |
| 20:45 | 4787 | Fortuna Sittard vs Twente | 3.40 | 3.55 | 1.94 |
| 21:30 | 5828 | Farul Constanta vs Rapid Bucuresti | 2.06 | 3.14 | 3.50 |
| 22:00 | 4462 | AZ Alkmaar vs Groningen | 1.31 | 4.91 | 8.02 |
| 22:45 | 1382 | Bologna vs Lazio | 2.90 | 3.05 | 2.39 |
| 23:00 | 1884 | Sparta Rotterdam vs Vitesse Arnhem | 2.35 | 3.25 | 2.80 |
| 23:00 | 3787 | Valencia vs Osasuna | 2.05 | 3.09 | 3.59 |
| 23:00 | 4789 | Brest vs Paris St Germain | 6.59 | 4.70 | 1.38 |
| 23:30 | 1877 | FC Vizela vs Sporting Braga | 3.67 | 3.47 | 1.91 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MINZIRO AZIPIGIA SALUTI TIMU ZA MAJESHI FA

**Na Hadija Mngwai**

KOCHA Mkuu wa Geita Gold, Fred Felix Minziro amesema kuwa haikuwa kazi rahisi kwake kuweza kutinga hatua ya robo fainali ya michuano ya kombe la FA kutokana na kukumbana na wakati mgumu na timu za majeshi.

Geita Gold ni miongoni mwa timu nane zilizotinga hatua ya robo fainali ya FA ikiwa inajipanga kuisaka hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo.

Akizungumza na Nipashe, Minziro amesema kuwa, anamshukuru Mungu kwa nafasi hiyo ambayo haikuwa kazi rahisi kuipata.

"Namshukuru Mungu kuweza kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali, haikuwa rahisi kufikia hapa tulipofikia, tumekutana na timu ngumu sana hasa za Majeshi Kama Green Warriors na Trans Camp. Hizi zote ni timu za Majeshi na ni ngumu kweli licha ya kuwa daraja la kwanza," alisema.

"Lakini namshukuru Mungu kwani nilikuwa na kikosi ambacho wachezaji wengi wameondoka, nina wachezaji wapya wengi hivyo vijana wameweza kupambana hatimaye tumeingia robo fainali kama mwaka jana.

"Kwa sasa tutapambana ili tuweze kufanikiwa kuingia katika hatua ya nusu fainali, wachezaji wangu wana hamasa kubwa kuhakikisha wanafanya vizuri," alisema Minziro.

Timu zilizofanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya FA ni pamoja na Simba, Yanga, Azam FC, Singida Big Stars, Mtibwa Sugar, Geita Gold, Mbeya City pamoja na Ihefu.



Wachezaji wa timu ya New Boys, Jonson Ashiraf (kulia), akiwania mpira dhidi ya Frank Meshak, wakati walipokuwa wakifanya mazoezi pembeni mwa uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Simba SC kunguruma Manungu*

INATOKA UK 24

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Mtibwa Sugar, Awadh Juma amesema kikosi chake kimejiandaa na pambano hilo, huku msemaji Thobias Kifaru alisema wachezaji wao watacheza mechi ya kwanza tangu wampoteze mchezaji wenzao, Idd Mobby aliyefariki Jumapili iliyopita kwenye Hospitali ya Benjamin Mkapa, baada ya kuugua kwa muda mfupi.

"Utakuwa mchezo mgumu kwetu kwa sababu wachezaji wetu bado watakuwa wanacheza wakimfikiria mwenzao, ila tutapambana na kama tukishinda basi utakuwa kwa heshima yake," alisema Kifaru.

Simba iko nafasi ya pili ka pointi 54, huku Mtibwa ikiwa kwenye nafasi ya tisa kwa pointi 29.

# Nabi aonya mastraika Yanga ikiivaa Geita Gold

INATOKA UK 24


Aidha aliongeza; "Nimezungumza na wachezaji wote katika eneo la mazoezi kwa sababu nataka watambue wazi kwamba tunachokifanya ni juu ya suala kutafuta ushindi, hatupaswi kucheza kwa ubinafsi wa aina yoyote kwa maana tunafuata malengo ya timu kuweza kufikia."

Alisema ana imani baada ya kuzungumza nao ataona mabadiliko kwenye mchezo dhidi ya Geita Gold kwa wachezaji wake kucheza kwa ushirikiano mkubwa ili kufikia malengo yao ya kutetea ubingwa wa Ligi Kuu na kucheza hatua ya robo fainali ya kombe la Shirikisho Afrika.

Nabi alisema wanahitaji kuendeleza walipoishia kwenye michezo ya ligi kuu kwa lengo la kuwa mbali kwa idadi za pointi.

"Tunahitaji kupata matokeo mazuri katika mchezo wetu wa Jumapili, utakuwa mgumu kwa sababu kila timu inahitaji kupata matokeo, sisi tunahitaji zaidi ili kuendelea kupishana kwa idadi kubwa ya pointi dhidi ya anayetufuatia, lakini matokeo hayo yataongeza molari ya wachezaji kuelekea mechi yetu ya US Monastir ya marudiano hapa nyumbani, " alisema Nabi.

Michezo
Nipashe
Jumamosi Machi 11, 2023



De Jong atangaza haondoki Barcelona UKURASA 21


Wachezaji wa Simba, Mohamed Husseini 'Tshabalala' (kushoto) na Henoc Inonga Baka wakichuana mazoezini jana. **PICHA: SIMBA**

## Nabi aonya mastraika Yanga ikiivaa Geita Gold

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga ikijiandaa na mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Geita Gold FC, utakaopigwa kesho Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi amesema hakufurahishwa na tabia ya ubinafsi iliyokuwa ikifanywa na baadhi ya wachezaji wake kwenye mchezo wa Kombe la Shirikisho dhidi ya Real Bamako ya Mali.

Hatua hiyo ni kufuatia mshambuliaji wao Fiston Mayele kuwa sehemu ya nyota hao kulazimisha kufunga mwenyewe katika nafasi alizokuwa anapata licha ya kutokuwa kwenye nafasi nzuri ya kufunga.

Katika hali hiyo Nabi ameendelea kusisitiza wachezaji wake kuachana na ubinafsi na kutaka mabadiliko kuanzia mchezo wao huo wa ligi kuu dhidi ya Geita Gold utakaopigwa katika uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema wamefanya maandalizi mazuri kujiandaa na mchezo huo na kuwahakikishia mashabiki watavuna pointi tatu muhimu ili kuendelea kuukaribia ubingwa.

Alisema licha ya mazoezi na maandalizi ya uwanjani, lakini pia anatumia muda wa kuongea na wachezaji wake kuachana na ubinafsi hasa washambuliaji wanapokuwa hawako nafasi nzuri ya kufunga na kutoa pasi kwa mtu ambaye yuko katika eneo zuri na kufunga.

"Nimelazimika kuwaeleza washambuliaji wote juu ya ubinafsi wa kulazimisha kufunga, mfano mechi iliyopita Mayele alifanya kosa hilo haikuwa kitu kizuri katika timu na nilimueleza wakati wa mapumziko kwamba hakufanya jambo zuri la yeye kulazimisha kufunga licha ya kutokuwa katika nafasi nzuri," alisema Nabi.

INAENDELEA UK 23

# Simba kunguruma Manungu

## ●●● Yajipanga kubeba pointi tatu dhidi ya Mtibwa Sugar, ili kupata molari ya kuivaa Horoya kwenye ...

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Simba kinashuka kwenye Uwanja wa Manungu Complex Turiani mkoani Morogoro leo kucheza na Mtibwa Sugar, ikiwa ni mechi ya raundi ya 24 ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayoelekea ukingoni.

**Simba itakuwa na kumbu kumbu mbaya ya kwenda kwenye uwanja huo Januari 22 mwaka jana katika mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu msimu iliopita na kulazimishwa suluhu, ikiwa ni moja ya pambano lililoipunguzia pointi za kuwania ubingwa ul iochukuliwa na Yanga baada ya misimu minne.**

Ni mechi ambayo ilichezwa kwenye uwanja uliojaa maji na matope kutokana na mvua kubwa iliyonyesha usiku wa kuamkia mchezo na asubuhi yake.

Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera alisema mechi itakuwa ngumu kwa sababu alivyoifuatilia Mtibwa Sugar amegundua ni moja kati ya klabu bora nchini, hivyo watakwenda kucheza kwa tahadhari kubwa.

Alisema wanataka kupata ushindi kwa ajili ya kuweka morali kuelekea kwenye mechi yao ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Horoya itakayochezwa Jumamosi ijayo Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Kupata pointi tatu kutoka kwa Mtibwa Sugar kutatupa morali kuelekea mechi ijayo ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Horoya AC. Tunataka kuendelea kupata matokeo bora, itatusaidia kujiamini zaidi," alisema kocha huyo.

Aliongeza; "Tunaifahamu Mtibwa Sugar, tunajua haitakuwa mechi rahisi kutokana na ubora walionao hasa kwa sababu watakuwa wanacheza uwanja wa nyumbani, tunahitaji matokeo chanya kwa ajili ya mchezo wetu wa Jumamosi na hii itakuwa na mambo mawili, kuhitaji ushindi, lakini inawapa wachezaji wangu morali kuelekea mechi yetu ijayo ya kimataifa."

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu ya Simba Ahmed Ally, amekuwa na hofu na hilo, akisema kama uwanja utakuwa mkavu basi mechi inaweza kuwa nzuri, lakini mvua ikinyesha itakuwa tabu tupu.

"Majeruhi wetu ni wale wale, Denis Kibu, Augustine Okra na Ismael Sawadogo, wengine waliobakia ni wazima, tunamshukuru Mungu mechi yetu dhidi ya Vipers haikuzalisha majeruhi yoyote. Tunacheza Manungu kiwanja fulani kigumu hivi ambapo mechi yetu ya mwisho tulitoka sare, kwa hiyo tunafahamu mechi ni ngumu na Mtibwa Sugar ni moja kati ya timu ngumu kwenye ligi yetu hii, hivyo tunakwenda kwa tahadhari kubwa," alisema.

"Kama mvua hazinyeshi na uwanja ukawa mzuri, naamini mechi nayo itakuwa nzuri, lakini kama ikinyesha, basi uwanja wa Manungu kama kawaida yake utakuwa na matope mengi kwa hiyo hali itakuwa ngumu kwa wachezaji. Pamoja na yote hayo, Simba tumejiandaa kwenda kuchukua pointi tatu mbele ya Mtibwa Sugar," aliongeza Ahmed.

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >